SUPA JACKPOT
TZS. 1,069,861,169
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Walimu** watatu walioshabikia kipigo cha mwanafunzi wahamishwa
UKURASA 3





# Nipashe

Ijumaa Januari 27, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581203

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




TISHIO UGAIDI

# Polisi yaipinga ripoti Marekani

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

**WADAU WAINGIWA HOFU MUSWADA WA HABARI KWENDA KWA DHARURA**

WADAU wa habari wameingiwa na hofu marekebisho ya Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016 kuwasilishwa...

UKURASA WA 10

**UVCCM YAONYWA LUGHA ZA MATUSI KWENYE MIKUTANO**

UMOJA wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), Mkoa wa Shinyanga, umetakiwa kuacha lugha za matusi...

UKURASA WA 15

**WATU 212 WAUGUA KIFAFA KILA MWAKA**

WATU 212 kila mwaka nchini hupata ugonjwa wa kifafa kunakosababishwa na kula nyama iliyoathirika na vimelea...



Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, akimsikiliza mmoja wa wagonjwa, Ramadhani Hamisi alipozuru Hospitali ya Taifa Muhimbili tawi la Mloganzila kujionea huduma inazozitoa mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: MAULID MBAGA**

## Ummy: Huduma zimeimarika Mloganzila

UKURASA 5

## Bilioni 50/- za mikopo hatarini kupotea kifisadi

UKURASA 2

**MICHEZO** **KAJULA AMRITHI BARBARA SIMBA** UK.24

**KATUNI** UK.6



Mchuuzi wa samaki akihudumia wateja wake Mbezi Mwisho Dar es Salaam jana, eneo ambalo hutumiwa pia na madereva wa bajaj hivyo wakati mwingine husababisha usumbufu. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Polisi yaipinga ripoti Marekani tishio ugaidi

**Na Mwandishi Wetu**

JESHI la Polisi limewatoa hofu wananchi dhidi ya tishio la ugaidi, likieleza kuwa matukio makubwa ya kihalifu ambayo yangeweza kuleta taharuki, yanadhibitiwa kuhakikisha hayatokei.

Taarifa hiyo ya polisi imekuja saa chache baada ya Ubalozi wa Marekani nchini kuwataka raia wake kuchukua tahadhari kutokana na kile ulichodai uwezekano wa kutokea uhalifu wa kigaidi kwenye maeneo yenye mikusanyiko mikubwa ya watu.

Taarifa ya Msemaji wa Jeshi la Polisi, David Misime, iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana, ilibainisha kuwa kutokana na taarifa hiyo ya ubalozi, polisi wameimarisha zaidi ulinzi na kwamba hali ni shwari.

Taarifa hiyo ya polisi ilibainisha kuwa udhibiti wa uhalifu unafanywa na jeshi hilo nchi nzima kama ambavyo makamanda wamekuwa wakitoa taarifa.

"Hata yale matukio ambayo yangetokea yameendelea kushughulikiwa kwa nguvu kubwa na wahalifu wameendelea kukamatwa kama makamanda wa polisi na vikosi wanavyoendelea kutoa taarifa zao mara kwa mara," alisema Misime.

Alisema jeshi hilo pia linaendelea kutoa elimu kwa wananchi kwenye maeneo mbalimbali ikiwa ni mkakati wake wa kukabiliana na uhalifu katika hatua za awali.

Kuhusu tahadhari ya tishio la uhalifu wa kigaidi iliyotolewa na Ubalozi wa Marekani, Kamanda Misime alisema tayari jeshi hilo limechukua hatua za kuimarisha ulinzi na usalama.

"Hivyo, tunatoa wito kwa wananchi kwamba hali ni shwari na waendelee na shughuli zao za kimaendeleo kama kawaida kwani Jeshi la Polisi tayari limeanza kufanyia kazi taarifa hiyo," alisema.

Aliwaomba wananchi kutoa taarifa kwa vyombo vya dola pale watakapomtilia shaka mtu au watu wanaoweza kusababisha uhalifu.

Taarifa ya Ubalozi wa Marekani iliyotolewa kupitia mitandao yake ya kijamii juzi, ilitoa tahadhari kwa raia wa nchi hiyo kwa kile kilichodaiwa kuwapo tishio la uhalifu wa kigaidi.

Taarifa hiyo iliwataka raia hao kuchukua tahadhari hasa kwenye maeneo yenye mikusanyiko mikubwa ya watu kama masoko na majengo makubwa ya ununuzi.

Taarifa hiyo ilidai kuwa walengwa wa uhalifu huo ni raia wa Marekani na wengine wanaotoka nchi za Magharibi wanaoishi nchini.

"Makundi ya kigaidi yanaweza kushambulia kwa tahadhari kidogo au bila ya taarifa, yakilenga hoteli, balozi, migahawa, maduka makubwa na masoko, vituo vya polisi, misikiti na maeneo mengine yanayotembelewa na raia wengi wa Magharibi," Ubalozi wa Marekani ulidai kupitia taarifa yake hiyo.


## NGOMENI ENTERPRISES

**NOTISI YA SIKU KUMI NA NNE (14) YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA.**

Kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na benki ya **CRDB BANK PLC** makao makuu Dar es salaam tunatoa notisi ya siku kumi na nne (14) tu ili uweze kulipa deni lako lote unalodaiwa Pamoja na gharama za dalali. Kukaidi au kushindwa kulipa deni hilo tutauza dhamana uliyoweka kwa mnada wa hadhara kama inavyoonesha kwenye jedwari hapo chini.

| S/N | JINA LA MDAIWA | DHAMANA / MAHALI | TAREHE/ MUDA |
|---|---|---|---|
| 1. | AVIT DAMACEN MLINDA | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO KIMARA STOP OVER YA UBUNGO, DAR ES SALAAM | 13.02.2023, KUANZIA SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA. |
| 2. | LAMECK JOHN RUGIGA & LEVINA METHEW TARIMO | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO MBEZI KWEMBE WILAYA YA UBUNGO, DAR ES SALAAM | 16.02.2023, KUANZIA SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 3. | KHARID RAJABU ABEDNEGO | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO VOKONGORO - CHANIAKA, WILAYA YA ILALA, DAR ES SALAAM | 20.02.2023, KUANZIA SA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 4. | REGINA ROMAN KAYOMBO | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO SARANGA MJII MPYA WILAYA YA UBUNGO, DAR ES SALAAM | 11.02.2023, KUANZIA SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 5. | HILLARY SYLVESTER JOSEPH | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO WAZO - KILIMAHEWA WILAYA YA KINONDONI, DAR ES SALAAM | 20.02.2023, KUANZIA SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA. |
| 6 | LEONARD ANDERSON MKONYI | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO, KIGURUNYEMBE MOROGORO YENYE HATI MILIKI NO.96142 | 25.02.2023, KUANZIA SAA 4 ASUBUHI NAKUENDELEA. |
| 7 | ARNOLD DOMINIC NYANGE& FORTUNATA ALPHAXAD MAGOMA | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO GOBA WILAYA YA UBUNGO DAR ES SALAAM. | 11.02.2023, KUANZIA SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 8 | KENNEDY CHRISTOSIAN MATHEMU | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO UKONGA MTAA WA MADAFU DAR ES SALAAM. | 10.02.2023, KUANZIA SAA 4 ASUBUHI |

**MASHARTI YAMNADA.**

1. Dhamana itauzwa kama zilivyo.
2. Mnunuzi atakayeshinda atalipa malipo ya awali ya asilimia 25 ya bei itakayofikiwa siku ya mnada na asilimia 75 atalipa ndani ya siku 14.
3. Mnunuzi atakayeshindwa kumalizia salio la asilimia 75 katika muda uliopangwa hapo juu, hatarudishiwa fedha alizolipa awali na mnada utarudiwa siku nyingine itakayopangwa.
4. Gharama zote za kubadilisha hati miliki, kutwaa nyuma na gharama nyinginezo zitakuwa juu ya mnunuzi.
5. Wateja wote mnakaribishwa kuona na kukagua nyumba muda wote isipokuwa usiku.

**MAWASILIANO:**
**CRDB BANK PLC HEAD QUARTER, NGOMENI ENTERPRISE DSM. SIMU: 0719974916/ 0784252048**


# Bilioni 50/- za mikopo hatarini kupotea kifisadi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) imebaini Sh. bilioni 50 kati ya Sh. bilioni 98 zilizotolewa kwenye mifuko ya uwezeshaji wananchi ni mikopo chechefu ambayo haiwezi kulipwa.

Kutokana na hali hiyo, kamati hiyo imemwagiza Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango kuwapa taarifa ili kujua walionufaika, maeneo waliko na wamenufaika kwa kiwango gani.

Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo, Japhet Hasunga, alibainisha hayo jana jijini hapo baada ya kukutana na Katibu Mkuu huyo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara na Baraza la Uwezeshaji la Taifa kujadili hoja za ukaguzi za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha 2020/21.

Alisema katika kikao hicho, wamejadili ripoti hiyo kuhusu mifuko ya uwezeshaji wananchi ambapo kwenye ripoti ilibainika kuwapo mifuko 52 ya serikali ambayo yote inafanya kazi mbalimbali.

"Kati ya mifuko hii ni pamoja na wa pembejeo za kilimo, mfuko wa kilimo kwanza, mfuko wa benki ya kilimo, mfuko wa kuwezesha wajasiriamali wadogo. Kamati imebaini kati ya Sh. bilioni 98 zilizotolewa, Sh. bilioni 50 ni mikopo chechefu ambayo haiwezi kulipwa," alisema.

Alisema kwenye Benki ya Maendeleo ya Kilimo imeonekana kuna zaidi ya Sh. bilioni saba ambazo zilitolewa na hazikwenda kwa walengwa waliokusudiwa.

"Tumemtaka Katibu Mkuu atupe taarifa kati ya mifuko hiyo, ni wanufaika wapi wamenufaika na wapo katika mikoa gani na kwa kiwango gani imewanufaisha," Hasunga alisema.

Hasunga ambaye ana taaluma ya ukaguzi wa hesabu za fedha, alisema kutokana na utendaji kutoridhisha kwenye maeneo yote ya mifuko hiyo, watalishauri Bunge hatua stahiki zichukuliwe kwa wale wote waliosababisha hasara.

Katika hatua nyingine, Kamati ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) imekutana na Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA) na kuitaka kuandaa mazingira rafiki ya utalii.

"Kuna barabara ambayo walipata kibali UNESCO ya kuijenga kwa tabaka la zege, sasa barabara ilivyo inafanya watu wengine kujutia, walipata kibali kwa teknolojia ambayo haiathiri hifadhi na kibali mwisho wake ni Desemba 2023, tunaishauri serikali kujenga barabara hii, itasaidia kuongeza kasi ya utalii," alisema Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Jerry Silaa.

## HABARI KITAIFA



Mwendesha bodaboda akiwa amebeba magunia ya mkaa akivuka daraja la muda lililoko Mto Mkomazi ambalo linaunganisha vijiji vya Wilaya za Korogwe na Handeni mkoani Tanga. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

# Sakata mwanafunzi kuchapwa, walimu watatu wahamishwa

**Na Lilian Lugakingira,**
BUKOBA

WALIMU watatu wa Shule ya Msingi Kakanja katika Wilaya ya Kyerwa mkoani Kagera walionekana kufurahia kitendo cha mwalimu mkuu wa shule hiyo kuwachapa watoto kwenye nyayo, wameamriwa kuhamishwa katika shule hiyo na kupelekwa sehemu nyingine.

Agizo la kuwahamisha lilitolewa jana na Katibu Tawala wa Mkoa wa Kagera, Toba Nguvila, kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa, baada ya kufika shuleni hapo na kufanya kikao na uongozi na watendaji mbalimbali wa ngazi ya kijiji, kata na wilaya.

Nguvila alisema pamoja na mamlaka nyingine ikiwamo Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kuendelea na uchunguzi juu ya tukio hilo, walimu hao hawapaswi kuendelea kuonekana katika maeneo ya shule hiyo na kuagiza wapelekwe walimu wengine wenye nidhamu nzuri waendelee na majukumu ya kuwafundisha watoto.

"Mkurugenzi pamoja na kuwahamisha walimu hawa kutoka katika hii shule, unapaswa kuendelea kuwafuatilia mwenendo wao na maadili yao katika maeneo ambayo watakwenda, lengo ni kuona kama wamebadilika na wanaendelea kutekeleza majukumu yao ya ulezi na ufundishaji vyema," alisema Nguvila.

Aidha, alisema madaraka ya Mratibu Elimu, Kata ya Kakanja, Sweetbert Kiiza, yamesitishwa tangu Januari 23, kwa kushindwa kutelekeza wajibu wake kama msimamizi wa elimu na nidhamu katika eneo lake na atapangiwa majukumu mengine.

"Haiwezekani jambo litokee tangu tarehe 10 Januari halafu wewe usiwe na taarifa nalo, lifike kwetu tarehe 23 Januari wakati nikiangalia kwenye kitabu naona umekwishafika hapa shuleni mara tatu, ina maana ulikuja kutalii kwa sababu kama ungekuja kwa ajili ya kukagua na kufanya vikao na walimu, ungechukua hatua haraka, kwa hiyo madaraka yako yamekwisha leo," alisema.

Nguvila alisema kwa kuwa kitendo alichokifanya mwalimu huyo cha kupiga watoto mpaka kuwajeruhi ni cha kijinai, Jeshi la Polisi liendelee na taratibu za kiuchunguzi ili hatua nyingine za kisheria zifanyike.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa, Stephano Ndabazi, alisema kuwa tukio hilo lilifanyika ndani ya ofisi ya walimu na walioadhibiwa kwa kosa la kutofanya kazi ya mwalimu ni watoto wanne, lakini ni mtoto mmoja aliadhibiwa kawaida katika makalio na wengine watatu wakapigwa kwenye nyayo huku wakiwa wamekanyagwa.

"Katibu tawala tumepokea maelekezo yako pamoja na kwamba kuna hatua zinaendelea kuchukuliwa na haya tunakwenda kuyafanyia kazi, lengo likiwa ni kuhakikisha tatizo kama hili halitokea tena katika shule hii, lakini katika shule nyingine," alisema.

Mwalimu Mkuu msaidizi wa shule hiyo, Devotha Alexender, alisema siku ya tukio akiwa shuleni hapo alifika ofisini kuwasalimia walimu wenzake na kukuta malalamiko dhidi ya mwalimu mkuu huyo, kuhusu njia aliyoitumia kuadhibu watoto hao.

"Nilikwenda kumweleza mwalimu mkuu namna anavyolalamikiwa na walimu kutokana na njia aliyoitumia kuadhibu watoto hao, akaniambia amenielewa na hatarudia tena kitendo hicho, lakini akaniomba niende kumwombea radhi kwa walimu wenzake kwamba limetokea tu na hatarudia tena," alisema.

Januari 10, mwaka huu, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Kakanja, wilayani Kyerwa, Issaya Emmanuel, aliwachapa watoto sehemu mbalimbali za miili yao ikiwamo kwenye nyayo za miguu, huku akiwa amewakanyaga kwa mguu wake, kwa kosa la kutofanya kazi (home work) waliyopewa wakati wakienda likizo.

Kutokana na kitendo hicho cha kikatili kilichofanywa na mwalimu huyo, ambaye alipigwa picha na kusambazwa mitandaoni, ameondolewa wadhifa wake wa kuwa mwalimu mkuu na kusimamishwa kazi ili kupisha uchunguzi.

# Utata waibuka mwili wa Mtanzania aliyefia Ukraine

**Na Christina Mwakangale**

MWILI wa Nemes Tarimo, Mtanzania aliyefia vitani Ukraine haujawasili na tarehe ya kuwasili haijulikani licha ya serikali kueleza mwanzoni mwa wiki kuwa ulikuwa umetolewa Russia asubuhi ya Jumanne wiki hii.

Mmoja wa wanafamilia ambaye hakutaka kutajwa jina gazetini, aliliambia Nipashe jana kuwa mpendwa wao anatarajiwa kuzikwa Tukuyu mkoani Mbeya lakini siku ya maziko haijatangazwa rasmi hadi mwili utakapowasili. Jumanne, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Stergomena Tax, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam kuhusu suala hilo, alisema Tarimo alikwenda Russia mwaka 2020, ili kujiunga na Chuo Kikuu cha Teknolojia Moscow (MIREA).

Alisema kuwa Machi 2022, Mtanzania huyo alihukumiwa kifungo cha miaka saba jela kwa mujibu wa sheria za Russia kutokana na vitendo vya uhalifu na baadaye wizara hiyo ilipokea taarifa kutoka huko kwamba kijana huyo alijiunga na kikundi cha kijeshi Russia kiitwacho Wagner.

"Tanzania hushirikiana na nchi mbalimbali duniani na wananchi huenda katika nchi hizo kikazi, kimasomo, kibiashara, shughuli za kiuchumi na kijamii. Nemes Tarimo alikwenda Russia na kujiunga na Chuo Kikuu cha Moscow Technology, mwaka 2020 kwa masomo ya Shahada ya Uzamili katika fani ya Teknolojia Habari za Biashara.

"Akiwa gerezani alipewa nafasi ya kujiunga na kikundi cha kijeshi cha Russia, Wagner kwa ahadi ya kulipwa fedha na kuachiwa huru baada ya kumaliza muda wa kutumikia vita.

"Alikubali kujiunga. Alifikwa na umauti Oktoba 24, 2022. Mwili umeondoka Urusi asubuhi hii (Jumanne)," alisema Dk. Tax na kubainisha serikali kupitia Ubalozi uliopo Russia, itaendelea kuwapa ushirikiano na kuhakikisha Watanzania, Diaspora, wanafunzi waliopo masomoni, wako salama wakati wote.

Kwa mujibu wa Katiba na sheria za Tanzania, raia wa Tanzania haruhusiwi kujiunga na jeshi lililoko nje ya nchi.

## NOTISI/TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD, NGOMENI AUCTION MART, REAL MASTER LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,YONO AUCTION MART &CO.LTD ,YARDLEY RECOVERIES AUCTION LTD, SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya Benki y**a AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,** tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| MBEYA | NJOLE NZALA MWASILE | GARI MITSUBISHI ROSA T557 DUV | GETRUDA BORANI MWAMLIMA | MBEYA | 30/01/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO |
| MOSHI | SHERAL SELEMANI HUSSEIN | GARI TATA BUS T357 DSR | SHERAL SELEMANI HUSSEIN | MBAGALA MAJIMATITU | 10/02/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | BRAITON REBEN MWANKEMWA | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | BRAITON REBEN MWANKEMWA | IVUMWE-MBEYA | 10/02/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | CHRISTOPHER JONSIA MSIGWA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | CHRISTOPHER JONSIA MSIGWA | MWANJELWA-MBEYA | 13/02/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | THOMAS JOSEPH KAPINGA | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | THOMAS JOSEPH KAPINGA | IGANZO-MBEYA | 14/02/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | FRENK SAMSON LEMAU | PAGALE LENYE HATI YA MAUZIANO | FRENK SAMSON LEMAU | SHEWA-MBEYA | 15/02/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | SALUM KONDO MWINYIMKUU | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NA. KNDOO 6783 | KONDO MWINYIMKUU | TANDALE MUHALITANI | 16/02/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| HEAD OFFICE | MOSES GODFREY MWAKALONGE | NYUMBA | MOSES GODFREY MWAKALONGE | MABWEPANDE | 23/02/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | SEBASTIAN SIMON SULUMO | NYUMBA | HAMADI MASUDI HASSANI | MBAGALA MAJIMATITU | 2/03/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | NEEMA CHRISTOPHER MICHAEL | NYUMBA | EMMANUEL MOGETA SAGI | KITANGWI-KISEMVULE | 2/03/2023 SAA 08:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| TEMEKE | MWAJUMA SHABANI MPONDI | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NA. TMK000450 | MWAJUMA SHABANI MPONDI | TOROLI - CHANG'OMBE | 9/03/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | YAKUB ISSA KIDUNDA | NYUMBA | YAKUB ISSA KIDUNDA | KIPUNGUNI-UKONGA | 16/03/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | JASMINI HAMIS ROBERT | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NA. KND 026532 | ROBERT KIRUGURO GIBAY | MABIBO-UBUNGO | 9/03/2023 SAA 08:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| TEMEKE | HAPPYNESS GEORGE MKOPI | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | PATRICK SAMWEL NGAYIWA | KIJICHI MGENI NANI | 13/02/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | NICE CHANDE MOHAMEDY | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI | ROSEMARY DESDELIUS HAULE | KWA AZIZI ALLY | 14/02/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | BUMERA LOGDE AND CO LTD | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI | JOACHIM HERONIMUS MWINGIRA | KIGOGO KATI | 15/02/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | IBRAHIM HARUNA MKALIPA | NYUMBA | IBRAHIM HARUNA MKALIPA | MBAGALA KIBURUGWA | 13/02/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | HOSEA MARCO OOKO | NYUMBA | KIBADENI J. NYATIENO | ZAVARA -ILALA | 21/02/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | DAUDI JAKAMUGAH MAKOSIGAH | NYUMBA | KIBADENI J. NYATIENO | ZAVARA -ILALA | 21/02/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | SEVERINI BONAVENTURA LYIMO | NYUMBA | SEVERINI BONAVENTURA LYIMO | MBEZI MTONI-MTONGANI | 15/02/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja,Gari au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.**0715868000/0714939933/0767809989**
4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.



Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Kanali Ahmed Abbas (katikati) akijaribu ubora wa trekta lililotolewa na Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) kwa Chama Kikuu cha Ushirika cha Masasi Mtwara (MAMCU) baada ya chama hicho kuibuka mshindi wa kampeni ya 'Vuna Zaidi na NBC Shambani' ya benki hiyo mahususi kwa mkoa wa Mtwara ikilenga kuchochea kiwango cha uzalishaji wa zao la korosho katika mkoa huo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wadau waingiwa hofu muswada wa habari kwenda kwa dharura

**Na Restuta James**

WADAU wa habari wameingiwa na hofu marekebisho ya Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016 kuwasilishwa bungeni kwa hati ya dharura kwa kuwa hadi sasa muswada haujawasilishwa kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria.

Mhariri Mtendaji wa Jarida la Fama, Neville Meena, aliiambia Nipashe jana kuwa muswada huo kutofikishwa kwenye kamati unawapa wadau wa vyombo vya habari nchini wasiwasi kama maoni yao yamezingatiwa.

Meena ambaye ni mwandishi mwandamizi na mjumbe wa Jukwaa la Wahariri (TEF), alisema muswada huo ungekuwa umewasilishwa kwenye kamati, ingewapa wadau fursa ya kuona maudhui yake na kutoa mapendekezo stahiki.

"Kupelekwa kwenye kamati, maana yake ni sisi tungeruhusiwa kuona content (maudhui) yake... mbaya zaidi mpaka tunavyozungumza sasa hivi, huo muswada haujapelekwa kwenye kamati," alidai Meena.

Alisema pamoja na hitilafu hiyo, serikali imetangaza kuuwasilisha bungeni katika Mkutano wa 13 wa Bunge unaotarajiwa kuanza wiki ijayo jijini Dodoma.

"Kama ulivyoona, waziri juzi alisema kuna vitu vilikuwa havijamaliziwa na wataalamu na wanavimalizia na kwamba watakwenda kwenye hatua inayofuata... ambacho sina hakika kama je, wataupeleka chini ya hati ya dharura?" alihoji Meena.

Makamu Mwenyekiti wa MISA-TAN, James Marenga, alisema sheria hiyo ina upungufu mwingi ambao wadau wanatamani ufanyiwe marekebisho ili kuruhusu ustawi wa vyombo vya habari nchini.

Alisema serikali imekubali kupokea marekebisho kadhaa ya wadau ikiwamo kuondoa jinai kwenye kosa la kashfa na sheria hiyo ina vifungu vinavyohitaji kurekebishwa.

"Uchochezi bado ni changamoto kubwa kwa sababu hauna tafsiri ndani ya sheria, kwa hiyo mwandishi ataandika habari gani ambayo sio ya uchochezi au ipi ni ya uchochezi?" Marenga alihoji.

Wakili wa Kujitegemea huyo pia alisema kifungu hicho kitabaki kilivyo, kitawaumiza waandishi kwa kuwa habari nyingi za uchunguzi zinaweza kutafsiriwa kuwa ni za uchochezi.

"Je, ni wakati gani mwandishi wa habari ataandika habari ionekane siyo ya uchochezi na nyingine ionekane ni ya uchochezi? Tafsiri ya uchochezi haikuwapo kwenye hiyo sheria na hatujui kama kutakuwa na mabadiliko," alisema.

Alivitaja vifungu vingine kwa vinavyohitaji marekebisho ni pamoja na cha kuundwa kwa Baraza Huru la Habari badala ya hivi sasa ambapo Baraza la Ithibati ndilo linalosimamia wanataaluma hao.

Kwa mujibu wa Marenga, jambo hilo linawanyima uhuru wanahabari kuwa na chombo huru kama zilivyo taaluma zingine kama wahasibu, wanasheria na wahandisi.

Marenga alitaja jambo lingine ni usajili wa magazeti kila mwaka na kwamba wadau wa habari wanapendekeza ifanyike kila baada ya miaka mitano.

"Suala la umiliki ni jambo ambalo linakwaza uwekezaji kwenye sekta ya habari kwa kuwa kwa mujibu wa sheria hiyo, mwekezaji wa nje ya nchi haruhusiwi kumiliki chombo cha habari kwa zaidi ya asilimia 49.

"Eneo la matangazo ni kikwazo kwani sheria hiyo inampa mamlaka Msemaji Mkuu wa Serikali kuamua matangazo yanayotoka kwenye taasisi za umma yatangazwe katika vyombo gani vya habari, jambo linalominya uhuru wa taasisi kuchagua chombo cha habari," alifafanua.

# Waziri aifariji familia ya askari aliyeuawa kwa mshale

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana, ametoa salamu za pole kwa familia ya Deus Mwakajegele, askari wa uhifadhi aliyekuwa akifanya kazi kwenye Hifadhi ya Taifa ya Serengeti aliyechomwa mshale wenye sumu wakati akitekeleza majukumu yake Nyanungu wilayani Tarime mkoani Mara.

Alitoa salamu hizo jana alipofika nyumbani kwa marehemu eneo la Ngongongale wilayani Arumeru mkoani Arusha baada ya kupata taarifa za kifo cha askari huyo ambaye enzi za uhai wake alijitoa kulinda wanyamapori kwa niaba ya Watanzania.

"Mimi kama Waziri mwenye dhamana ya Maliasili na Utalii nimekuja hapa kutoa pole kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki pamoja na jumuiya yote ya wahifadhi.

"Nimepokea kwa masikitiko makubwa kifo cha kijana wetu aliyeshambuliwa kwa kupigwa mshale wenye sumu siku ya Jumamosi tarehe 21, 2023 wakati akitekeleza majukumu yake," alisema waziri huyo.

Kufuatia hali hiyo, Balozi Dk. Pindi alitumia fursa hiyo kukemea vikali vitendo vya baadhi ya wananchi wanaojichukulia sheria mkononi huku akisisitiza kuwa Jeshi la Uhifadhi liko imara na litaendelea kulinda maeneo yote ya hifadhi kwa faida na manufaa ya kizazi cha sasa na baadaye.

Alibainisha kuwa tayari mtu aliyehusika na tukio lililosababisha kifo cha askari huyo tayari ameshakamatwa huku wengine walioshirikiana naye, wanaendelea kusakwa ili sheria ichukue mkondo wake.

Mjomba wa Marehemu, Sisito Kigongo, alisema kuwa askari huyo alikuwa ni mhimili kwa familia, hivyo kifo chake kimekuwa pigo kubwa kwa familia, mpwa wake huyo akiacha watoto watatu.

# Pesapal yaja na suluhisho usimamizi vituo vya mafuta

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya huduma za malipo ya Pesapal imeanzisha huduma mpya ya kusaidia kusimamia uendeshaji wa vituo vya mafuta na mauzo ya nishati nyingine inayotumia teknolojia za kisasa na kufanya kazi kisasa.

Viongozi wa kampuni hiyo wamebainisha kuwa lengo kuu la suluhisho hiyo ni kuwasaidia wamiliki wa vituo hivyo kupunguza gharama za uendeshaji na kuongeza ufanisi kwenye biashara ya rejareja ya mafuta.

Kupitia teknolojia hii, Pesapal imejipanga kuhakikisha hadi mwisho wa mwaka huu vituo vya mafuta 100 kwenye masoko ya Tanzania, Kenya na Uganda vitakuwa vinatumia mfumo huo mpya.

Kitaalamu na kibiashara suluhisho hili linajulikana kama Pesapal Forecourt Management Solution (PFMS). Katika taarifa kwa vyombo vya habari iliyotolewa juzi jijini Dar es Salaam, kampuni hiyo ilisema PFMS ndilo jibu la matakwa ya wenye vituo vya mafuta kuwa na muunganiko wa vifaa vya mauzo usiokuwa na hitilafu yoyote.

Taarifa hiyo ilibainisha kuwa PFMS pia ina uwezo mkubwa wa kusimamia na kufuatilia kwa karibu jinsi uuzaji mafuta unavyofanyika. "Uwezo huu ndio unalipa suluhisho hili sifa ya kupunguza gharama za uendeshaji, pia kusaidia kuondokana na ulaghai huku ikiboresha namna wateja wanavyohudumiwa kwa mawanda mapana ya koungeza mauzo.

"Suluhisho la PFMS linawezesha wamiliki wa vituo vya mafuta kufuatilia na kusimamia bila kuwapo vituoni mauzo ya gesi na mashine za kujazia mafuta, mfumo wa vipimo vya matangi, bodi za bei na jinsi malipo yanavyofanyika," Pesapal ilibainisha katika taarifa yake hiyo.

Februari mwaka jana Pesapal ilipata kibali cha kutoa suluhisho jumuishi za malipo kwa vituo vya mafuta kutoka kwa Jukwaa la Kimataifa la Viwango (IFSF). Taasisi hiyo ni jumuiya ambayo imejikita zaidi kufanikisha kuwapo teknolojia za viwango vya kimataifa kwa ajili ya kusaidia kuboresha uendeshaji wa vituo vya mafuta ya magari na nishati nyingine.

Akizungumza kwenye utambulisho wa PFMS katika masoko ya ukanda huu, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Pesapal Limited, Agosta Liko, alibainisha umuhimu wa kuufanya mchakato mzima wa usimamizi wa mafuta kuwa wa kiotomatiki.

Alisema uwekezaji huo hutengeneza mazingira madhubuti katika sekta ya rejareja ya mafuta na kuimarisha eneo mtambuka la biashara hiyo kwa hasa kupunguza gharama za uendeshaji na kuimarisha huduma kwa wateja.

Liko alisema matumizi ya suluhisho ya PFMS ili kusaidia zaidi kurahisisha malipo kwenye vituo vya kuuzia mafuta, yatafanyika kwa ushirikiano wa kimkakati kati ya Pesapal na wamiliki wa vituo husika.

"Katika nyanja inayobadilika kwa kasi kama hii ya usimamizi wa kuuza mafuta rejareja, kunahitajika suluhisho ambalo ni la kisasa na linaloanzisha mienendo mipya ya kufanya mambo," alisisitiza.

Kwa mujibu wa Meneja wa Pesapal Tanzania, Bupe Mwakalundwa, mbali na suluhisho yao kuwa bunifu zaidi, pia linazingatia zaidi kuwapa wenye biashara ya vituo vya mafuta uwezo wa kuboresha huduma kwa wateja na kuwahudumia watu wengi kwa ufanisi mkubwa.

"Hili suluhisho huwapa wateja fursa ya kufanya ununuzi wao kwa mkupuo wa muamala mmoja, huku wasimamiaji wa vituo vya mafuta wakiwezeshwa kuidhinisha miamala haraka na kwa usalama," alisema Bupe. Pesapal Limited ni kampuni ya huduma za malipo inayohusika na zana za kuchakata malipo zikiwamo za kidijitali na kimtandao hususani kwa ajili ya mashirika ya kibiashara na taasisi nyingine zenye mwelekeo huo.

Pesapal ilianzishwa mwaka 2009 na kwa sasa inafanya biashara katika nchini sita za Kiafrika ambazo ni pamoja na Zambia, Zimbabwe and Malawi.

Kwa Tanzania, kampuni hiyo imekuwapo tangu Julai mwaka jana baada ya kupata idhini ya Benki Kuu kutoa huduma za malipo yasiyohusisha fedha taslimu chini ya Sheria ya Mifumo ya Malipo ya Taifa ya Mwaka 2015.

HABARI KITAIFA

# Waziri Ummy: Huduma afya zimeimarishwa Mloganzila

**Na Maulid Mmbaga**

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu (pichani), amesema huduma zinazotolewa kwenye Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) Tawi la Mloganzila zimeimarishwa.

Amesema hospitali hiyo kwa sasa ina madaktari bingwa na vifaa vya tiba vya kutosha pamoja na miundombinu rafiki kwa wagonjwa, wauguzi, ndugu wanaowatembelea na wafanyakazi.

Akizungumza jana mkoani Dar es Salaam alipozuru hospitalini huko kukagua huduma zinazotolewa, Waziri Ummy alisema wamehamishia idara tatu kutoka Muhimbili za magonjwa ya kisukari, moyo na afya ya akili.

“Niwatoe wasiwasi wananchi ukiambiwa mgonjwa wako aende Mloganzila, usiseme hapana kwa sababu siyo tu ameletwa daktari mmoja au wawili, wameletwa madaktari wote wa ile idara, wauguzi wao pamoja na wataalamu wote wanaohusiana na hiyo idara.

“Tumehoji baadhi ya ndugu wa wagonjwa wenyewe, wengi wamefurahia kwamba huduma sasa Mloganzila ni nzuri, na mimi ninataka kusema kwa kweli ninaridhishwa na utoaji huduma kwenye hospitali yetu ya Mloganzila na mpaka sasa VVIP wanalazwa hapa,” alisema Ummy.

Aliongeza kuwa kwenye hospitali hiyo, wataalamu na vifaa vipo, akibainisha kuwa baada ya miaka mitano wataangalia utaratibu wa kurudisha huduma hizo Muhimbili Upanga ili kote ziwapo kutokana na wingi wa watu.

Alielekeza taasisi zote za afya za serikali kuhakikisha kama kuna maendeleo yoyote wanataka kufanya au kuanzisha huduma, waende kuzianzisha Mloganzila, ili kuleta muungano na uwiano wa huduma zinazotolewa katika hospitali hiyo.

“MOI wanataka kujenga kituo cha huduma Mbweni, hapana waje huku ili tuwe na muungano wa huduma. Kwa hiyo kama hawajafika mbali, ninawapiga ‘stop’, tuje huku tuna eneo hekta 3,800 kwa sababu lazima hizi huduma zihusiane,” aliagiza.

Alipongeza uongozi wa hospitali hiyo kwa kuwa na ongezeko la wangonjwa wanaokwenda kupata huduma katika hospitali hiyo kutoka 9,595 mwezi Julai 2022 hadi 13,224 kwa wagonjwa wa nje na wa kulazwa kutoka 857 hadi 1,246, sambamba na ongezeko la mapato.

Waziri huyo alimpongeza Mkurugenzi wa MNH, Prof. Mohamed Janabi, kwa usimamizi na kazi nzuri anayoifanya katika kuhakikisha huduma bora zinatolewa hospitalini huko, akibainisha kwamba ana mpango wa kuorodhesha Mloganzila kwenye orodha ya hospitali za umma.

Waziri Ummy pia alitoa maelekezo kwa uongozi wa Hospitali ya Taifa Muhimbili kutoa maelezo ya kufafanua ni wangonjwa wa magonjwa gani wanapaswa kwenda tawi la Mloganzila na ni wepi waende Upanga, ili kuepuka usumbufu wa kuzunguka na wagonjwa.

Maelekezo hayo yalikuja baada ya mmoja wa wagonjwa waliokuwa wakitibiwa Mloganzila kufikisha malalamiko hayo kwa Waziri Ummy, kwamba wanapata usumbufu wa kwenda Upanga na kurudi kwenye hospitali hiyo kutokana na aina ya magonjwa wanayougua.

Grece Steven, mmoja wa wagonjwa wakiokuwa wakitibiwa hospitalini huko, aliwashukuru wataalamu wa afya kwa kuwahudumia vizuri.



**BIMA YA AFYA**

Akizungumzia suala la Bima ya Afya kwa Wote, Waziri Ummy alisema wamejipanga kwa kuongeza miundombinu ikiwamo ujenzi wa zahanati, vituo vya afya, hospitali, ununuzi wa vifaa tiba vya kisasa na kuongeza idadi ya watumishi na kwamba kilichobaki ni utayari wa wananchi kujiunga na huduma hiyo.

“Tunataka mnavyomhudumia mgonjwa katika hospitali za binafsi ndivyo hivyo tumhudumie akiwa kwenye hospitali ya umma na ikiwezekana tuweke mazingira mazuri kwenye hospitali za umma badala ya daktari baada ya muda wa kazi kuhangaika kwenda huku na huku, vijiwe zaidi ya vinne kwa siku, afanye shughuli zake za binafsi palepale.

“Muhimu ni kukubaliana asilimia ngapi itaingia kwake na ngapi kwa taasisi, ninataka kuwaahidi chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan sambamba na majengo na vifaa tiba, hatutaacha kuweka kipaumbele kwenye rasilimali watu, wataalamu wa afya, hilo tutalisisitiza kwa kiasi kikubwa,” alisema Ummy.


## FIRST HOUSING FINANCE (TANZANIA) LIMITED
## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

1st Housing

### IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31.12.2022

*(Kiasi kwa shilingi elfu)*

| | | Robo Mwaka ya sasa 31st Dec. 2022 | Robo Mwaka iliyopita 30th Sept. 2022 |
|---|---|---|---|
| A. | MALI | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 1,532 | 114 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | - | - |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 3,596,769 | 3,653,121 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 6,686,677 | 7,490,847 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 19,782,685 | 18,702,590 |
| 12 | Mali Nyingine | 706,751 | 751,697 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 1,622,000 | 1,622,000 |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 323,876 | 303,223 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **32,720,290** | **32,523,592** |
| | | | |
| B. | B. DHIMA | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | - | - |
| 18 | Amana za Wateja | 911,787 | 741,689 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 630,360 | 809,745 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 332,190 | 291,964 |
| 27 | Dhima Nyingine | 385,116 | 359,665 |
| 28 | Madeni | 12,003,729 | 12,001,976 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **14,263,182** | **14,205,039** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI *(16 kutoa 29)*** | **18,457,107** | **18,318,554** |
| | | | |
| C. | FEDHA ZA WANAHISA | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 21,800,000 | 21,800,000 |
| 32 | Malipo juu ya bei ya hisa | - | - |
| 33 | Akiba ya Mtaji | 95,831 | 95,831 |
| 34 | Mapato Yaliyobakizwa | (3,678,678) | (3,691,652) |
| 35 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 239,954 | 101,401 |
| 36 | Akaunti Nyingine za Mtaji | - | 12,974 |
| 37 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **38** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **18,457,107** | **18,318,554** |
| 39 | Dhima Zisizo Dhahiri | - | - |
| 40 | Mikopo Chechefu | 595,259 | 486,216 |
| 41 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 182,969 | 104,434 |
| 42 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| | | | |
| D. | BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 56.41% | 56.32% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 2.98% | 2.58% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 2063.47% | 2439.66% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 60.46% | 57.50% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 88.31% | 91.68% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 22.93% | 17.46% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 0.60% | 0.89% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31.12.2022

*(Kiasi kwa shilingi elfu)*

| | Maelezo | Robo ya Mwaka sasa | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) | Limbikizo la Mwaka wa sasa | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 31st Dec. 2022 | 31st Dec. 2021 | 31st Dec. 2022 | 31st Dec. 2021 |
| 1 | Mapato ya Riba | 1,079,165 | 671,466 | 3,668,523 | 2,487,835 |
| 2 | Gharama za Riba | (336,596) | (32,158) | (1,000,506) | (122,779) |
| 3 | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **742,568** | **639,308** | **2,668,017** | **2,365,056** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (78,535) | (51,003) | (127,321) | (17,041) |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **82,623** | **90,113** | **341,118** | **130,606** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | (1,616) | (1,616) | (1,480) | (1,464) |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 73,386 | 48,784 | 240,122 | 53,781 |
| | 6.3 Gawio | - | - | 27,590 | 35,130 |
| | 6.4 Mapato Mengine | 10,853 | 42,946 | 74,885 | 43,159 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(599,385)** | **(556,375)** | **(2,619,191)** | **(2,229,229)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (368,932) | (378,592) | (1,390,844) | (1,165,923) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (230,452) | (177,783) | (1,228,347) | (1,063,306) |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **147,272** | **122,043** | **262,624** | **249,392** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (8,718) | (7,321) | (22,669) | (16,430) |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **138,554** | **114,721** | **239,954** | **232,962** |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | - | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa robo ya mwaka /mwaka** | **138,554** | **114,721** | **239,954** | **232,962** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 23 | 19 | 23 | 19 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 0.64 | 0.53 | 1.10 | 1.07 |
| 15 | Idadi ya Matawi | 1 | 1 | 1 | 1 |
| | | | | | |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.42% | 0.55% | 0.74% | 1.12% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 0.75% | 0.63% | 1.30% | 1.28% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 72.64% | 76.28% | 87.04% | 89.32% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 2.53% | 3.37% | 2.53% | 12.89% |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31.12.2022

| *(Kiasi kwa shilingi elfu)* | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Robo ya mwaka ya sasa (31.12.2022)** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa robo ya mwaka (01.10.2022)** | **21,800,000** | **-** | **(3,590,252)** | **12,974** | **-** | **95,831** | **18,318,554** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 138,554 | - | - | - | 138,554 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | 12,974 | (12,974) | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa robo ya mwaka (31.12.2022)** | **21,800,000** | **-** | **(3,438,724)** | **-** | **-** | **95,831** | **18,457,107** |
| | | | | | | | |
| **Robo ya mwaka iliyopita (30.09.2022)** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka (01.07.2022)** | **21,800,000** | **-** | **(3,615,871)** | **11,956** | **-** | **95,831** | **18,291,915** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 26,638 | - | - | - | 26,638 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (1,019) | 1,019 | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa robo ya mwaka (30.09.2022)** | **21,800,000** | **-** | **(3,590,252)** | **12,974** | **-** | **95,831** | **18,318,554** |


### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31.12.2022

*(Kiasi kwa shilingi elfu)*

| | | Robo ya Mwaka sasa | Robo ya Mwaka iliyopita | Limbikizo la Mwaka wa sasa | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 31st Dec. 2022 | 30th Sept. 2022 | 31st Dec. 2022 | 31st Dec. 2021 |
| I: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | **147,272** | **31,938** | **262,624** | **249,392** |
| | **Marekebisho kwa Ajili ya:** | - | - | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | 40,661 | 158,579 | 286,856 | 321,866 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (1,139,203) | (2,367,105) | (6,338,723) | (7,376,039) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 170,099 | 110,243 | 423,700 | 75,000 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (136,378) | 129,989 | 275,678 | (50,276) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 63,716 | 44,211 | (108,153) | (44,042) |
| | - Kodi iliyolipwa | (18,770) | (10,052) | (22,669) | (12,917) |
| | - Mengineyo | 32,739 | 57,985 | 67,950 | (5,640) |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **(839,863)** | **(1,844,211)** | **(5,152,738)** | **(6,842,656)** |
| II: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| | Gawio Lililopokewa | - | - | 27,590 | 35,130 |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (2,207) | (73,170) | (34,804) | (48,243) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 56,352 | (57,721) | 4,870 | (1,059,492) |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **54,146** | **(130,891)** | **(2,344)** | **(1,072,605)** |
| III: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Deni jipya kutoka CRDB Bank | 1,753 | 4,850 | 10,993,044 | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | (49,021) | (73,531) | (95,154) |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **1,753** | **(44,170)** | **10,919,513** | **(95,154)** |
| | | | | | |
| IV: | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| | **Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu** | **(783,964)** | **(2,019,273)** | **5,764,431** | **(8,010,415)** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 7,490,961 | 9,510,546 | 945,786 | 8,921,409 |
| | Badiliko Halisi Katika Mikopo ya mabenki | (18,788) | (313) | (22,009) | 34,792 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka** | **6,688,208** | **7,490,961** | **6,688,208** | **945,786** |

### MINIMUM DISCLOSURES OF CHARGES AND FEES

| S/No | ITEMS | CHARGES/FEES |
|---|---|---|
| 1 | Prime Lending Rate (PLR) | 16% p.a. |
| 2 | Maximum spread above PLR | 4% p.a. |
| 3 | Application Fee (Non-refundable) | TZS 200,000/- |
| 4 | Processing Fee | 1.5 % of the loan value |
| 5 | Facility Fee | 1.5 % of the loan value |
| 6 | Valuation Fee | Paid by the client as per the invoice |
| 7 | Legal Fee | Paid by the client to FHF account and FHF will pay law firm |
| 8 | Early Repayment | 5% of the amount to be prepaid |
| 9 | Annual Review Fee | NIL |
| 10 | Cheque returned Unpaid (Outward & Inward) | TZS 50,000/- |
| 11 | Loan Statement | TZS 20,000/- |




Katika kuanda taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8).

| Jina na Cheo : | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Sasa M. Chonza **(Ofisa Mtendaji Mkuu)** | **(Imesainiwa)** | **25.01.2023** |
| Amulike E. Kamwela **(Mkuu wa Fedha)** | **(Imesainiwa)** | **25.01.2023** |
| Isambo Binde **(Mkaguzi Mkuu wa Ndani)** | **(Imesainiwa)** | **25.01.2023** |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi).

| Jina: | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| **Conrad Dsouza** Mwenyekiti | **(Imesainiwa)** | **25.01.2023** |
| **Vinod Rustagi** Mkurugenzi | **(Imesainiwa)** | **25.01.2023** |

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Adhabu wanazotoa walimu zichunguzwe

**SERIKALI** ya Mkoa wa Kagera, imefikia uamuzi wa kumsimamisha kazi Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Kakanja ya mjini Bukoba, baada ya kuonekana kwenye video fupi iliyokuwa ikisambaa kwenye mitandao ya kijamii, akiwaadhibu wanafunzi wake kwa kuwachapa viboko kwenye nyayo zao huku akiwa amemkanyaga mmoja wao miguuni.

Uamuzi huo uliotolewa na Mkuu wa Mkoa wa Kagera, tunasema unastahili kwa sababu kitendo alichokifanya mwalimu huyo ambaye ni mkuu wa shule kuwa ni cha kinyama.

Tunasema adhabu zinazochukuliwa kinyume na haki za binadamu ni lazima zichunguzwe ili kukomesha tabia hiyo inayofanywa na baadhi ya walimu.

Adhabu hizo zinaweza kuathiri watoto si kimwili tu hata kisaikolojia na kuwafanya wachukie shule na kusababisha kuwa na taifa la watoto wasiokuwa na elimu.

Unapompiga mtoto kwenye maeneo ambayo yanaweza kumletea ulemavu ni kwenda kinyume na haki za binadamu.

Kwa tukio hilo na mengine mengi yanayojitokeza kwenye baadhi ya shule kwa kutoa adhabu kali na zingine za udhalilishaji ni lazima hatua za haraka zichukuliwe kukomesha.

Kama kusingekuwa na mwalimu aliyechukua video hiyo na kuirusha kwenye mitandao ya kijamii, ina maana tukio hilo lingenyamaziwa na mwalimu huyo angeendelea kuathiri watoto wengine.

Kuna umuhimu wa kufanya uchunguzi hata kwa kuongea na watoto kujua madhila wanayopitia kutoka kwa walimu wao ili hatua zichukuliwe.

Tunaona hatua pia zimechukuliwa kwa walimu wengine wa Shule ya Msingi Kakanja, walionekana kufurahia adhabu aliyokuwa akitoa mwalimu mkuu kwa wanafunzi hao.

Hatua hizo ni kuhamishwa katika shule hiyo na kupelekwa sehemu nyingine. Lakini tunaona kuhamishwa sio suluhisho kwa sababu hata huko wanakokwenda wanaweza kuendeleza tabia hiyo.

Iliamriwa kuwa pamoja na mamlaka nyingine ikiwamo Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kuendelea na uchunguzi juu ya tukio hilo, walimu hao hawapaswi kuendelea kuonekana katika maeneo ya shule hiyo na kuagiza wapelekwe walimu wengine wenye nidhamu nzuri waendelee na majukumu ya kuwafundisha watoto.

Pia madaraka ya Mratibu Elimu, Kata ya Kakanja, yamesitishwa tangu Januari 23, kwa kushindwa kutelekeza wajibu wake kama msimamizi wa elimu na nidhamu katika eneo lake na atapangiwa majukumu mengine.

Hili la watu kufanya makosa na kupangiwa majukumu mengine tunaona linawafanya watu kuwa na kiburi kwa sababu ya kujua kuwa watapewa kazi nyingine na kuendelea kupata mshahara.

Wanaofanya makosa hayo wanapaswa kupewa adhabu kali ili wajutie kile walichokifanya na pia iwe fundisho kwa wengine.


Mwalimu Mkuu msaidizi wa shule lilipotokea tukio, alieleza wazi kuwa akiwa shuleni hapo alifika ofisini kuwasalimia walimu wenzake na kukuta malalamiko dhidi ya mwalimu mkuu huyo, kuhusu njia aliyoitumia kuadhibu watoto hao.

| Telegraphic Transfer - Normal Customer (SWIFT) | | | 55.00 | 55.00 | |
| TISS- Normal Customer | | | 10,000.00 | 4.20 | |
| TISS-Staff | | | 6,000.00 | 2.10 | |
| LOAN PRODUCT LENDING RATES | | | TZS | USD | |
| MICRO LOANS (Rahisi Loans) TZS 500,000 to 10,000,000 | | | from 66% to 72% Based on risk profile/risk group of client | N/A | |
| MICRO LOANS TZS 10,000,001 to 35,000,000 | | | from 46.8% to 60% Based on risk profile/risk group of client | N/A | |
| AGRO LOANS TZS 500,001 TO 35,000,000 | | | from 49.2% to 74.4% Based on risk Profile/Risk Group of client | N/A | |
| SME LOANS/ODs 35,000,000 to 200,000,000 | | | from 26.4% to 33.6% Based on risk profile/Risk Group of client. | N/A | |
| Loans/OD Secured by Fixed Term Deposits | | | 20.40% | N/A | |
| Loan Processing Fee | | | TZS | USD | |
| MICRO LOANS (Rahisi Loans) TZS 500,000 to 10,000,000 | | | 3.40%Inclusive of excise duty and VAT | N/A | |
| MICRO LOANS TZS 10,000,001 to 50,000,000 | | | 3.40%Inclusive of excise duty and VAT | N/A | |
| AGRO LOANS TZS 500,001 TO 50,000,000 | | | 3.70%Inclusive of excise duty and VAT | N/A | |
| SME LOANS/ODs 35,000,000 to 200,000,000 | | | 2.90%Inclusive of excise duty and VAT | N/A | |
| Loans/OD Secured by Fixed Term Deposits | | | 1.5% Inclusive of excise duty and VAT | N/A | |
| Application Fee | | | TZS | USD | |
| MICRO LOANS (Rahisi Loans) TZS 500,000 to 10,000,000 | | | 20,000.00 | N/A | |
| MICRO LOANS TZS 10,000,001 to 50,000,000 | | | 20,000.00 | N/A | |
| AGRO LOANS TZS 500,001 TO 50,000,000 | | | 20,000.00 | N/A | |
| SME LOANS/ODs 35,000,000 to 200,000,000 | | | 20,000.00 | N/A | |
| Loans/OD Secured by Fixed Term Deposits | | | 20,000.00 | N/A | |
| Insurance Fee | | | TZS | USD | |
| MICRO LOANS (Rahisi Loans) TZS 500,000 to 10,000,000 | | | 1.5% | N/A | |
| MICRO LOANS TZS 10,000,001 to 50,000,000 | | | 1.5% | N/A | |
| AGRO LOANS TZS 500,001 TO 50,000,000 | | | 2.0% | N/A | |
| SME LOANS/ODs 35,000,000 to 150,000,000 | | | 1.5% | N/A | |
| Loans/OD Secured by Fixed Term Deposits | | | 1.5% | N/A | |





## Wadau wa bima watakiwa kuwafichua wabadhirifu

**Na Elizabeth Faustine,** MWANZA

KAMPUNI za bima nchini zimetakiwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizoko ili kufichua ubadhirifu unaofanywa na watu wasiofuata utaratibu.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Kamishna wa Bima Nchini, Dk. Baghayo Saqware, wakati wa mkutano wa pili wa wadau wa bima uliofanyika jijini Mwanza kwa lengo la kusikiliza malalamiko, kutathmini na kupokea maoni mbalimbali juu ya huduma zinazotolewa na mamlaka hiyo.

Dk. Saqware alisema matarajio yao ni kuona wananchi wengi Kanda ya Ziwa wanapata huduma ya bima kwa lengo la kulinda mali zao, afya na bima zingine huku watoa huduma wakizingatia kanuni na taratibu za utoaji wa huduma hiyo.

"Unapopewa leseni na mamlaka wewe ni msaidizi wa mamlaka ili kutoa huduma na kuisaidia mamlaka kufichua ubadhirifu, hivyo hatutegemei mtoa huduma aliyepewa leseni avunje sheria na kanuni za bima au taratibu za bima tulizojiwekea," alisema Dk. Saqware.

Aliongeza kuwa serikali inategemea ushauri wa wadau na kupokea maoni ya wananchi wanaohudumiwa ili kutatua matatizo yanayowakabili.

"Ndugu wadau na wananchi mliofika hapa serikali inategemea kupitia watoa huduma ya bima za umma na binafsi kuweka jitihada na mifumo thabiti ya kuzuia udanganyifu na ubadhirifu wa kibiashara katika soko huria, hivyo watoa huduma wa umma na binafsi tunategemea mtaongeza wigo wa usambazaji wa huduma na upatikanaji wake kwa kutumia uweledi wenu," alisema.

Dk. Saqware alisema lengo la serikali ni kuona wananchi wanaohudumiwa na bima wanafikia asilimia 18 mwaka 2025, huku mchango wa sekta ndogo ya bima katika pato la taifa ukiongezeka na kifikia asilimia tatu mwaka 2030.

# UVCCM yaonywa lugha za matusi mikutano ya hadhara

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

UMOJA wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), Mkoa wa Shinyanga, umetakiwa kuacha lugha za matusi kwenye mikutano ya hadhara, badala yake washindane kwa hoja na kueleza wananchi miradi ya maendeleo ambayo imefanywa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Ushauri huo ulitolewa jana Mjini Shinyanga na Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, kupitia UVCCM, Ramadhani Mlao, wakati wa maadhimisho ya miaka 46 ya kuzaliwa kwa chama hicho.

Alisema Rais Samia ameruhusu kuanza kwa mikutano ya hadhara, hivyo vijana wa UVCCM wajipange mguu sawa kukitetea chama pamoja na Rais kwa kuwaeleza wananchi juu ya miradi ya maendeleo ambayo imetekelezwa.

"UVCCM ndiyo askari wa CCM, tumlinde Rais wetu na kukitetea chama, wapinzani wakitutukana matusi kwenye mikutano ya hadhara sisi tujibu hoja na siyo kujibu matusi, kwa sababu tuna mambo mengi ya kuwaeleza Watanzania nini ambacho CCM imefanya," alisema Mlao.

Kadhalika, aliwataka vijana wa UVCCM kuanzisha miradi ya maendeleo ikiwamo kujikita kwenye kilimo ili wawe na uchumi imara na kufanya mambo yao kwa uhuru na siyo kuburuzwa na kuwa vibaraka wa watu.

Aidha, alitembelea kituo cha watoto wenye ulemavu kilichoko Buhangija katika Manispaa ya Shinyanga na kuwapa pole ya kuunguliwa na mabweni yao mawili ambayo yalisababisha vifo vya watoto watatu. Akiwa katika kituo hicho alitoa msaada wa vitu mbalimbali ikiwamo sabuni za unga, mafuta ya kujipaka, juice na biskuti.

Naye Mwenyekiti wa UVCCM, mkoani Shinyanga, Clement Madinda, alisema maelekezo yote yaliyotolewa na mjumbe huyo watayafanyia kazi ikiwamo kuanzisha miradi ya kiuchumi.

Aliipongeza serikali kwa kuendelea kuwaamini vijana na kuwapatia mikopo mbalimbali ili kujikwamua kiuchumi, kwamba katika Manispaa ya Shinyanga vikundi viwili vya vijana vimepewa gari mbili na Kahama wamepewa trekta mbili na wanaendelea na shughuli.

Aliwaomba maofisa maendeleo ya jamii kuendelea kutoa elimu ya ujasiriamali kwa vijana na namna ya kutumia fursa ya mikopo ya halmashauri ikiwamo kuanzisha miradi yenye tija na kujikwamua kiuchumi.

Meya wa Manispaa ya Shinyanga, Elias Masumbuko, aliwaasa vijana wa CCM wasibweteke badala yake watumie fursa ya mikopo ya halmashauri kuanzisha miradi ya kiuchumi.




Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Shinyanga wakiwa na Mjumbe wa Halmashauri Kuu wa chama hicho kupitia kundi la vijana, Ramadhani Mlao, wakitoa msaada wa vitu mbalimbali zikiwamo sabuni za unga za kufulia, mafuta ya kujipaka, juice na biskuti katika kituo cha kulea watoto wenye ulemavu mbalimbali Buhangija Manispaa ya Shinyanga walipowatembelea kuwapa pole ya kuunguliwa na mabweni na kupoteza wenzao watatu. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Afariki dunia kwa kushambuliwa na watu wasiojulikana

**Na Rose Jacob,** MWANZA

MKAZI wa eneo la Ghana wilayani Ilemela, Yusuph Kassim (55), amefariki dunia baada ya kuvamiwa na watu wasiofahamika kumshambulia kwa kumkata na kitu chenye ncha kali kichwani wakati akiwa shambani kwake katika Kijiji cha Chabula wilayani Magu mkoani Mwanza.

Akizungumzia tukio hilo Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Mwanza, Wilboard Mutafungwa alisema Januari 23, mwaka huhu, Yusuph alikwenda katika shamba analofuga ng'ombe, samaki na ilipofika saa 3:00 usiku akiwa na kijana wake ambaye ndiye mwangalizi wa eneo hilo alianza kukagua shamba lake.

"Wakati wakiendelea na shughuli ya kutembelea shamba hilo, ghafla walivamiwa na watu watatu waliokuwa wameficha nyuso zao ambao walianza kumshambulia, huku kijana wake akifanikiwa kuwatoroka wauaji hao na kujificha ufukweni mwa ziwa," alisema Kamanda Mutafungwa.

Alisema kijana huyo alitoa taarifa kwa wananchi na viongozi walianza msako wa kumtafuta, kufanikiwa kumpata akiwa amefariki pembeni mwa bwawa la samaki, huku akiwa na jeraha kubwa kichwani.

Kamanda Mutafungwa alisema askari polisi kwa kushirikiana na kitengo cha uchunguzi wa sayansi ya jinai mkoani Mwanza lilifika katika eneo la tukio na kufanya ukaguzi kuhusiana na mauaji hayo.

Kamanda Mutafungwa alisema: "Chanzo cha mauaji hayo bado hakijajulikana, tunaendelea na msako wa kuwatafuta watu waliohusika, mwili wa marehemu umehifadhiwa katika Hospitali ya Wilaya ya Magu".



Ukurasa 12

Kilivyo kilimo mseto mnazi cha kisasa, kutoka kazi ya watafiti TARI




Ukurasa 13

Tukiwa na serikali yenye rais na mawaziri wawili, itakuwaje?

BUFE

IJUMAA JANUARI 27, 2023

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



Ukurasa 14

## Rais Samia katika staili ya mipango uchumi akiwekeza ughaibuni, nyumbani kwa mpigo

# SBL na mikakati mipya, kuwajibikia jamii kupitia mazingira, elimu kilimo

**Na Frank Monyo**

MOJA ya kanuni na sheria za uwekezaji nchini ni kinachoitwa 'corporate social responsibility' kwa maana namna mashirika yanavyojikimu kijamii.

Hapo ina maana suala la uwekezaji, linaendana na namna linavyorejesha faida au manufaa kwa jamii hasa katika maeneo jirani. Yapo yanayojenga shule au kuzawadia umma miradi ya kiuchumi na biashara.

Sasa kuna asasi zinatoa majibu hayo kwa namna yake, yakielekezwa katika sura pana ya maisha, ikiwamo mbinu za kilimo bora na cha kisasa, usalama kazini, kutunza mazingira na usalama wa umma, pia barabarani.

Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL) imo kwenye wanaowekeza katika kilimo bora, pia mazingira, jamii na utawala (ESG), ikiwa ni sehemu ya uwakibikaji huo katika jamii, ikifafanuliwa ni sera ya kampuni kuendesha biashara zake.

Mkurugenzi wa Uhusiano wa Umma wa SBL, John Wanyancha, anasema mifumo ya ESG ni muhimu katika uwekezaji endelevu, kwa sababu inawasaidia kutambua jinsi kampuni yao inavyoweza kupanga misingi ya thamani yao, kuchambua mchango wake katika jamii.

"SBL pia imefanya juhudi kukuza sekta ya kilimo ambapo kupitia programu yake ya Kilimo Viwanda, inayotoa fursa kwa wanafunzi wanaotoka katika familia zenye kipato cha chini, zaidi ya wanafunzi 200 wamefaidika na masomo ya kilimo, ambayo huwafanya kurudi katika maeneo yao kusaidia wakulima kutekeleza shughuli zao kitaalamu," anaeleza.

Wanyancha anaendelea: "Wiki chache kabla ya kufunga mwaka 2022, SBL ilizindua Ripoti yake ya Uendelevu chini ya kampuni mama ya East African Breweries Limited (EABL) iliyokuwa ikionyesha utendaji mzuri wa uzalishaji unaoendana na ESG.

"Ukweli ni kwamba, kampuni haziwezi shupaza shingo bila kuweka umuhimu wa kufuata misingi ya kimazingira, kijamii na taratibu za kiutawala... tunategemea kuendeleza mpango huu na kutimiza malengo mengi," akitamka kuwa hadi sasa kunapunguzwa kwa asilimia kubwa utupaji taka za kiwandani, hakuna inayoenda dampo.

SBL nchini ina viwanda katika miji ya Mwanza, Moshi na Dar es Salaam, pia eneo lingine la utekelezaji wao kwa mazingira linagusa kupunguza matumizi yasiyo ya lazima, ikipunguzwa matumizi ya maji kwa asilimia 7.6 sawa na lita milioni 40 katika viwanda vyake vyote vitatu.

Ni hatua ambayo inavuka viwango vya mwaka 2021, ikifikia asilimia 98, wakati lengo lilikuwa kuzuia matuzi ya maji kwa asilimia 90, pia ikishiriki kupanda miti 5,000 mkoani Dodoma.

Inaelezwa, mwaka 2023 kampuni imeendesha kampeni ya kuhimiza usalama barabarani na uendeshaji makini, wakiwafikia madereva 5,130 nchi nzima.

Vilevile anasema, SBL imefanikiwa kufikia jamii kupitia mfumo wake wa kielektroniki ikitoa elimu ya matumizi ya pombe kwa zaidi ya watu 2,900 na kutoa elimu kwa wanafunzi takribani 8,200, kuhusu ubaya wa unywaji pombe katika umri mdogo.

Meneja wa Kanda ya Mashariki wa Baraza la Mazingira Tanzania (NEMC), Hamadi Kissiwa, anataja kwenye uzinduzi wa Ripoti ya Uendelevu ya SBL mwaka jana, anaonyesha mfano muhimu wa wawekezaji kwa kuzingatia mazingira na masuala ya tabianchi, akitoa mfano wa sekta ya maji.

Anafafanua kuwa "(SBL) inatambua umuhimu wa rasilimalii hiyo nyeti katika uzalishaji wa bidhaa zake na jamii kwa kujenga miundombinu ya kutibu maji mkoani Manyara katika Kijiji cha Basuro, wilayani Hanang."

Pia anasema miundombinu hiyo ya kutibu maji ina uwezo wa kuhudumia watu 14,000 na kutibu takribani lita 900,000 za maji ndani ya saa 12. Mradi huo wa maji unawafikia watu katika vijiji vinne ndani ya Kata ya Basuto.




Aliyekuwa Spika wa Bunge, Job Ndugai, akimwagilia mti alioupanda wilayani Kongwa, hatua iliyofadhiliwa na Kampuni ya Bia Serengeti. Wanaoshuhudia ni wananchi na watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa. **PICHA: MTANDAO**

UCHUMI

# Kilivyo kilimo mseto mnazi cha kisasa, kutoka kazi ya watafiti TARI Mikocheni

**Na Mwandishi Wetu**




MINAZI ni zao muhimu kitaaluma katika kilimo na hata kijamiii. Ni zao linaloanza kulimwa mseto sasa na wakulima wadogo.

Kimsingi, minazi inalimwa kwenye maeneo yenye ukubwa wa hekta 265,000, zaidi katika ukanda wa Pwani nchini na visiwani Zanzibar. Pia kuna maaeneo mengine yanakolimwa minazi, mikoani Kigoma, Wilaya ya Kyela - Mbeya na Mwanza kwenye fukwe za Ziwa Viktoria.

Inatajwa ni zao linalostawi vizuri katika maeneo yenye nyuzi joto 27, pia mvua milimita 2,000 inayotawanyika vizuri, zaidi ya asilimia 75 ya unyevunyevu, jua la kutosha na kwenye udongo unaopitisha maji kirahisi.

**TEKNOLOJIA INAYOTUMIKA**

Kuna teknolojia inayotumika kwa wadau wa kilimo cha minazi. Asasi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) kupitia Kituo cha Utafiti wa Kilimo Mikocheni (TARI-Mikocheni) kwa kushirikiana na halmashauri zote kunakolimwa zao hilo.

Mpango mkakati wa kuendeleza zao la minazi, umejikita katika kufanya utafiti na kusambaza teknolojia zinazogunduliwa na watafiti wa kilimo, mfano ni matumizi bora ya mbinu za kilimo, kama mbegu bora za minazi zinazostahimili ukame na zinazokinzana na magonjwa na wadudu; kilimo mseto; matumizi bora ya mbolea; pia utunzaji bora wa mashamba kulingana na mabadiliko ya tabianchi.

Watafiti wa Kituo cha Utafiti wa Kilimo Mikocheni, sasa wamekuja na teknolojia ya kilimo mseto, kinachochanganya kilimo cha minazi na mazao mengine kama mihogo, michungwa, miembe, viazi lishe, mazao ya jamii ya kunde, ndimu, mahindi, nyanya na mboga.

Kilimo cha minazi kinatajwa kukubaliana sana na mfumo mseto, kwa sababu kuna nafasi kubwa kati ya mstari kwa mstari na mnazi hadi mnazi. Watafiti wa Kituo cha Utafiti wa Kilimo Mikocheni kwa kushirikiana na mradi wa Fruits and Vegetables for Sustainable Healthy Diet (FRESH), wamekuja na kilimo mseto kati ya minazi na mboga; mchicha, mnavu na nyanya chungu.

Mashamba darasa ya kilimo mseto, yamefanyika katika wilaya nne ambazo ni Bagamoyo, Ilala, Kigamboni na Mkuranga.

Wilayani Mkuranga, mashamba darasa yamefanyika mawili, moja kwa mkulima na lingine Kituo Kidogo cha Utafiti cha Mikocheni-Mkuranga). Dhumuni kubwa la mradi huo ni kuhakikisha wanufaika wanapata lishe bora itakayoboresha afya zao, pia kuwahakikishia usalama wa chakula.

> **“Vilevile kuna kuhamasisha na kutangaza kilimo cha zao la minazi, pia mengineyo katika mnyororo wa thamani, ikiwa na maana ni mfumo mzima wa uzalishaji, usindikaji na mauzo yake.**



Sehemu ya mbegu za minazi zinazopatikana kwenye ofisi za TARI Mikocheni, Dar es Salaam.

Ni mradi unaolenga kuboresha maisha, pia kuwawezesha wanawake na vijana na kupunguza athari zitokanazo na mazingira. Umeanza kutekelezwa kwa kuanzishwa mashamba darasa, ili kuhamasisha matumizi na ulaji wa mboga; kusambaza teknolojia za mboga kwa wadau mbalimbali wa kilimo.

Teknolojia hizo ni kama: Utambuzi wa aina ya mbegu za mboga zilizoboreshwa kiutafiti, ambazo ni jamii ya mchicha katika makundi ya: Pori na Akeri, kwa ajili ya nafaka; hali kadhalika Nguruma kwa ajili ya majani.

Yako pia mazao yanayoorodheshwa kitaalamu; mnavu, ambureni, nyanya chungu, tengeru white na DB3.



Wakurugenzi wa TARI, Dk. Joseph Ndunguru wa Mikocheni (kushoto) na Mkurugenzi Mkuu, Dk. Joseph Mkamilo, pia Mratibu Mkuu, Dk. Fred Tairo, wakimkabidhi mkulima Asha Msangi wa Wilaya ya Mtama, Lindi miche bora ya minazi aina ya Eat. **PICHA ZOTE: MAKTABA**

**MAANDALIZI YALIVYO**

Kunatajwa suala la uanzishwaji na kuandaliwa kitalu cha kuruhusu upandaji sahihi, kwa sababu upandaji mbegu zilizoboreshwa, unahitaji kuwa katika vitalu na nafasi kubwa.

Pia hiyo teknolojia inatajwa inafaa kufundishwa kwa sababu na uzoefu unaonyesha, utaratibu wa kuupanda, unajumuisha kumwaga mbegu na sio kupanda kwa mistari.

**MATUMIZI SAHIHI**

Hapo inajumuisha matumizi bora kwa kupanda kwa nafasi, kanuni bora za kilimo cha mboga inajumuisha kuweka mbolea, kumwagilia, kupalilia na kupunguza mimea

Uvunaji; kuna suala la kuiongezea thamani mboga, mfano zao la mnafu linatumika kukausha mboga; mchicha nafaka kwake inatumika kutengeneza bisi, unga wa uji na vitafunwa mbalimbali

Baada ya mashamba darasa hayo kufanyika kati ya watafiti na wadau wa kilimo katika wilaya hizo nne, tathmini ya mashamba darasa ilifanyika kupata mboga bora, kati ya hizo zote zilizopandwa.

Mfano hai unatajwa katika mboga mchicha ulioko wa aina tatu, kwa maana ya mwanzo wa mradi kulikuwa na mbegu aina tano na baada ya utafiti na tathmini, zikabaki aina tatu zinazofaa na ndizo zilizopandwa katika kipindi cha pili cha mradi huu.

Hadi sasa, tathmini ya matokeo bado inafanyiwa kazi na pindi majibu yatakapopatikana, wadau watajulishwa. Baada ya kufanya tathmini hizo Kituo cha TARI-Mikocheni kwa kushirikiana na mradi wa “FRESH” waligawa mbegu bora zilizotafitiwa kwa wakulima na wadau mbali mbali walioshiriki katika siku ya mkulima katika wilaya zote nne.

**MENEJA TARI MIKOCHENI**

Akielezea teknolojia ya kilimo mseto kilivyo, Dk. Fred Tairo, Meneja wa Kituo cha Utafiti wa Kilimo Mikocheni, Dar es Salaam, anasema kilimo hicho kina lengo la kumwinua mkulima wa minazi kiuchumi na kumpatia tija maradufu zaidi ya kutegemea kilimo cha minazi pekee.

Mbegu zilizogawiwa ni mchicha aina ya ‘Nguruma, Poli na Akeri’ kwa upande wa nyanya chungu ni ‘DB3’ na ‘Tengeru White’ ni mnavu. Hadi sasa, TARI Mikocheni imeshagawa mbegu za Ambureni zote zikiwa zimetafitiwa na ziko vizuri katika mavuno.

Mmoja wa waliootesha mbegu hizo awali, Samweli Wapili Mwombezi, ambaye akapata mafunzo ya kupima uwezo wake kutoka Kituo cha Mafunzo ya Wakulima Pugu Kinyamwezi, Wilaya ya Ilala, Dar es Salaam, anasema watafiti wamewakomboa kwa kuwaletea mbegu bora.

Anaelezea mtazamo wake kwamba ni mbegu zitakazowakomboa wakulima hata wakapata mavuno mengi, huku wakiboresha afya zao kujipatia kipato chja ziada.

Pia anawashauri wakulima wenzake, kuhusu umuhimu wa kutumia mbinu bora za kilimo cha mboga ambazo ni kupanda kwa mstari, kutumia mbolea na dawa za kuua wadudu kwa wakati, ili kupata matokeo chanya.

**UMUHIMU KILIMO MSETO**

Kilimo mseto kinatajwa kuwa muhimu sana na kinasaidia kuongeza rutuba kwenye udongo, hivyo kinaongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na mazao mengine shambani.

Vilevile kinatajwa kuongeza kipato kitokacho shambani, kwa kuwa aina mbalimbali za mazao hupatikana kwa mara moja, huku kikisaidia kupunguza uharibifu wa mazingira, pale miti inaponyonya hewa chafu ya kaboni angani.

Manufaa mengine ni kwamba inapunguza gharama za kurutubisha ardhi, ikilinganishwa na njia nyinginezo za matumizi ya mbolea za viwandani.

Pia mbadala huo una nafasi ya ziada kwamba, minazi ni chanzo cha upatikanaji malighafi za viwanda na nishati kwa ajili ya jamii.

Kwa mujibu wa TARI Mikocheni, kilimo cha mseto cha kuchanganya minazi na michungwa, miembe, ndimu ni muhimu kwa sababu mazao hayo ni makazi ya wadudu rafiki wa mkulima waitwao maji moto (weaver ants).

Wadudu hao wanawadhibiti wadudu waharibifu kwenye minazi kama vile mbu wa minazi (coconut mites na coconut bugs), hivyo kwa kutumia kilimo mseto, mkulima anapunguza matumizi ya viuatilifu shambani kwake.

**MTAZAMO WA KITAALAMU**

Mara zote, matarajio ya mkulima atakapofanya kilimo mseto, ni kushuhudia tija shambani, kwa maana ya uzalishaji unaojitosheleza na endelevu katika upatikanaji mazao na chakula, vilevile kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na ardhi ya kilimo, unaowaongezea wakulima kipato.

Kituo cha Utafiti Kilimo - Mikocheni, sasa kinanuia kupeleka ufahamu kwa wakulima kuhusu kilimo cha minazi na hilo linafanyika kuwajengea uwezo wakulima kwa njia ya mafunzo, mashamba darasa, semina na mikutano.


Vilevile kuna kuhamasisha na kutangaza kilimo cha zao la minazi, pia mengineyo katika mnyororo wa thamani, ikiwa na maana ni mfumo mzima wa uzalishaji, usindikaji na mauzo yake.

Ni jambo linaloendana na kuendelea kufanya utafiti mbalimbali unaolenga kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili wakulima wa zao la minazi.

***• Uchambuzi huu wa kilimo, unatokana na andiko, pia kazi ya kitaalamu ya watafiti wa Kituo cha Utafiti Kilimo - Mikocheni, Dar es Salaam.***

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Tukiwa na serikali yenye rais na mawaziri wawili, itakuwaje?






**NA JOSEPH KULANGWA**
**(+255) 713 410008**
**kulangwasos@gmail.com**

SIJUI kwanini siku za karibuni, nimejikuta nina taswira na njozi zinazofanana, kuhusu nchi nitakayoiumba na kuja na serikali isiyofanana na zingine duniani! Nadhani ni maono tu chanya.

Ni maono yanayonijia kutokana na jinsi dunia yenyewe inavyokwenda, ikiwa imegubikwa na mabadiliko ya tabianchi yanayotishia, hata uhai wa sayari hii katika miaka mingi ijayo, hata kutabiri mwisho wake.

Dunia hii inapitia kipindi kigumu, ambacho kinawafanya wanadamu kufikiria mengi ya kufanya, hasa katika kuhakikisha wanamudu maisha na kukabiliana na mabadiliko yoyote yanayowaathiri.

Binadamu wanaelewa hilo, kwamba huenda kukatokea janga kubwa linalosababishwa na mabadiliko ya tabianchi, ambayo yanachagizwa na uharibifu wa mazingira, unaotokana na ukataji miti holela na shughuli zingine za kibinadamu.

Wanadamu kwa kuwa waliambiwa na Mungu wao, kwamba ‘enendeni mkaijaze dunia na kutawala kila kilichomo,’ basi wakaona hakuna namna, ila kutawala viumbe kwa kuwawinda, kuwachinja na kuwala.

Wengine kwa kuwavua na wengine kwa kuwakatakata na kuwatumia kwa mapishi ya waliowaua, ili kukamilisha mlo, bila ya kujali kuwa kumbe kukata miti na kuigeuza nishati ya kupikia kuna madhara yake.

Madhara makubwa ni kukosekana hewa safi, pia kuzuia mvua kunyesha na kusababisha ongezeko la hewa ukaa na endapo hali hii itaendelea kwa takriban miaka 100 ijayo, hakuna ajuaye lini utakuwa mwisho wa dunia na hakuna atakayeushuhudia.

Wanasema hakuna ajuaye mwisho wa dunia nini kitatokea, lakini kama hakutakuwa na mvua, ina maana hakutakuwapo kilimo cha kuzalisha chakula, kwani ardhi itakuwa imekauka, hakioti kitu na hewa ukaa itakuwa imetaradadi kila mahali.

Kuna vilio duniani kote kuhusu hali hii na kitakachojiri baadaye na ndiyo maana, kila mmoja katika nchi yake anatafuta jinsi ya kukwepa, kama si kuondokana na hali hii, ambayo madhara yake hayatapata wa kuyasimulia, kwani hakutakuwa na viumbe hai. Katika mazingira kama haya, ndiyo sababu nimekuja na maono ya kuwa na serikali itakayoongozwa na watu watatu tu na wasaidizi wao, ambao ni Rais na mawaziri wawili tu. Hilo bila shaka kwa tuliozoea mawaziri zaidi ya 20 litakuwa maajabu.

Nikiulizwa ni mawaziri gani hao nitakaotaka wawe katika serikali hiyo ya kufikirika? Nitajibu kifua mbele kuwa ni wa Kilimo na wa Afya. Kwanini? Kwa sababu bila ya kilimo hakuna chakula na bila chakula hakuna uhai. Hali kadhalika, bila ya afya hakuna uhai.

Serikali hii hata kama itakuwa ya muda mfupi, lakini italenga katika kuhakikisha inabana matumizi na kupanga mipango ya kuendesha kilimo chenye tija, kwa kuelekeza nguvu zote katika kusimamia mazingira na kulima kwa kumwagilia.

Serikali hii italenga kuhakikisha kila mmoja anapata huduma ya afya ili awe timamu na nguvu muda wote wa kufanya kazi mashambani na kujipatia chakula na lishe, ili kujipanga kukaribisha wizara zingine zikihitajika.

Wapo watakaohoji kwanini kuwa na wizara mbili tu, huku nchi ikihitaji mambo mengi yakiwamo ya usalama, uhusiano kimataifa, ulinzi, elimu, michezo, utawala bora na mengine ya aina hiyo.

Watajibiwa, kuwa wote hao wanategemea chakula na utimamu wa afya ili kuyatekeleza hayo, kwa maana kwamba hayo mengine yatatekelezwa na wananchi wenyewe, kulinda nchi na kukabiliana na wahalifu wataachiwa wananchi kuyakabili.

Serikali itajikita katika kuhakikisha wakulima wanapata mahitaji yote ya msingi, yatakayowawezesha kulima kwa tija, ili chakula kiwepo muda wote na kwa utoshelevu, huku madaktari wakihakikisha kuwa nguvukazi haiugui ovyo.

Hapo wananchi ambao ndio walengwa, watakuwa na nguvu ya kupambana na maadui wa ndani na nje ya mipaka, wananchi hao hao kwa kiwango chao cha elimu watafundisha watoto wao, watajitawala chini ya rais wao atakayekuwa akiwaonyesha njia.

Ifahamike kuwa, daktari asiye na taaluma ya ualimu anaweza kuwa mwalimu akamfundisha mtoto au mtu yeyote kusoma, kuandika, kuhesabu, pia sayansi, lakini mwalimu asiye na taaluma ya udaktari, hawezi kwenda hospitali kutibu mgonjwa hata iweje. Ndiyo msingi wa hoja yangu ya kuenzi madaktari.

Kuhusu uhusiano wa kimataifa, hilo litakuwa mikononi mwa Rais na wasaidizi wake wa karibu atakaowateua ikimpendeza. Hiyo ndiyo itakuwa serikali ya nchi hii katika kipindi hiki cha mpito kuelekea kujinasua na hali mbaya ya mabadiliko ya tabianchi. Njooni na mawazo mbadala msinipopoe. Alamsiki!

UCHUMI

# Rais Samia katika staili ya mipango uchumi akiwekeza ughaibuni, nyumbani kwa mpigo

• Mabalozi kila mmoja akumbushwa wajibu wake

**Na Mwandishi Wetu**

TANGU kuingia kwenye wadhifa wa sasa, Rais Samia Suluhu Hassan akichukua nafasi ya marehemu, John Magufuli, kuna mambo kadhaa yamekuwa yakibeba nafsi yake zaidi, hata mwenyewe akiyatolea ufafanuzi au kuyatenda.

Mosi, amekuwa Makamu wa Rais kwenye utawala wa marehemu Rais Magufuli, wote wakitoka kwenye Chama Cha Mapinduzi (CCM), ambayo imekuwa ikiongoza nchi kihistoria na mfumo wao wa utendaji uongozi kichama 'kupokezana kijiti' kwa falsafa na mambo yao ya pamoja.

Hata hivyo, ni kawaida kuwapo tofauti ya nafsi na hulka, kati ya awamu moja ya madaraka na nyingine, hata kuwafanya viongozi hao wasifanane katika baadhi ya mambo yao katika kuiwajibikia umma.

Kiutendaji, hilo lililishawahi kufafanuliwa na Rais wa Awamu ya Pili, Mzee Ali Hassan Mwinyi, aliyehamisha nchi kutoka mfumo wa kiuchumi huria mwaka 1985, pia kisiasa miaka saba baadaye nako kukaondoka kutoka mfumo hodhi, akifafanua kwa msemo 'kila zama na azma zake.'

Hasa kiuchumi, ndicho kilichoko sasa hatua ya kukabidhiana kijiti kwa ajenda ileile kitaifa na ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM, bado uongozi mpya una maono yake ndani ya mstari wa zamani kifalsafa, itikadi, sera na msimamo.

Hata hivyo, ndani yake kunakuwapo mabadiliko ya nafsi na muda ukiegemea 'kila zama na azma zake.' Hapana shaka, sura ya mama na haki ya jinsia katika utawala wa Rais Samia, umekuwa na nafasi kubwa kuanzia hamasa hadi uteuzi, huku ukiibua upya maendeleo ya kijinsia uongozi wa Tanzania, ambayo pia ni ajenda ya dunia.

**SURA YA MIRADI**

Eneo mojawapo ambalo amekuwa akiliwekea mkakati kivitendo ni katika miradi mikuu miwili ya kitaifa, ambayo pia ilimpa sifa kubwa mtangulizi wake, Marehemu Magufuli.

Rais Samia, ambaye ni sehemu ya miradi hiyo kwa maana ya kuwa Makamu wa Rais, akabuni kaulimbiu 'Kazi Iendelee' kurithi ya mtangulizi wastani wa miaka mitatu iliyopita 'Hapa Kazi tu' iliyodumu zaidi ya miaka mitano.

Moja ya hatua aliyoanza nayo 'kupokeza kijiti', akiahidi atatekeleza ya mtangulizi wake kwa kuyaendeleza, ambayo sasa kunashuhudiwa kama kama alivyoahidi wakati anapewa madaraka. Hapo kwa nafasi ya pekee kunatajwa mradi wa treni ya umeme, maarufu SGR na mradi mkubwa wa umeme kitaifa na Afrika wa Mwalimu Nyerere.



Mabalozi wa Tanzania waliokusanyika Zanzibar, miezi kadhaa iliyopita wakimsikiliza Rais Samia Suluhu Hassan. **Chini;** Rais Samia alipokuwa akiwahutumia maofisa hao. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

> **"Kuna wakati zilimfikisha Rais Samia nchi za mbali, ambazo hazikuishia mafanikio kiuchumi na kibiashara pekee, bali kuja na pesa za moja kwa moja kuhudumia miradi.**

Hadi sasa, ripoti za utekelezaji miradi zinaonyesha ndani ya miaka mitatu ya uongozi wa Rais Samia, mradi mkubwa wa Umeme wa Julius Nyerere aliyoukuta ujenzi ukiwa katika wastani wa asilimia 20, sasa uko asilimia 80.

Hatua iliyopo inatajwa ni kujaza maji mabwawa yake, kazi iliyoanza hivi karibuni na kitaalamu inaelezwa inahitaji misimu mwili hadi mwaka 2024 ili kuanza kazi, wakati hatua za kukamilisha mradi kwa asilimia 20 zilizobaki, unatarajiwa kukamilishwa kutimu mwakani.

Pia mradi wa reli SGR ambao Rais Samia alianza madaraka ujenzi ukiwa wastani wa asilimia 80 kipande cha Morogoro na Dar es Salaam, sasa umeshakamilishwa, kazi ikiendelea kukamilishwa kipande kati ya Dodoma na Isaka, Tabora na huduma za treni hiyo nazo zinatarajiwa kuanza ndani ya kipindi si kirefu sana.

**ALIVYOJIPANGA**

Moja ya mitihani kwa Rais Samia, ni hatua kama ilivyo nchi nyingi zilizoko harakati za kusaka maendeleo, ni namna ya kupata fedha za kufanikisha miradi kukamilika.

Kama ilivyowasilishwa katika makala kama hii wiki iliyopita, moja ya mikakati ni kubuni mipango ya urafiki jirani na ughaibuni kusafisha mazingira ya kibiashara, kama ilivyoshuhudiwa na ziara ya nchini Kenya.



Rais Samia akarejea nchini akiwa amefuta orodha ya vikwazo vya biashara jirani, baada ya kukutana na aliyekuwa Rais wakati huo, Uhuru Kenyatta.

Pia ziara kama hizo za mafanikio na kuifungua milango, inagusa nchi nyinginezo za Afrika Mashariki na mbali; Rwanda, Ethiopia, Burundi, Uganda, Afrika Kusini, Namibia, Malawi na Zimbabwe.

Kuna wakati zilimfikisha Rais Samia nchi za mbali, ambazo hazikuishia mafanikio kiuchumi na kibiashara pekee, bali kuja na pesa za moja kwa moja kuhudumia miradi.

Hapo kulipatikana fedha za msaada kiasi cha Euro milioni 450 sawa na shilingi trilioni1.17 kutoka Umoja wa Ulaya (EU), ikiwa sehemu ya Euro bilioni 55 zilizotengwa na umoja huo kwa ajili ya Afrika kukabiliana na janga la Covid 19.

Kimsingi, ndio fedha zilizopangwa katika kipindi cha miaka mitatu ijayo, kukwamua miradi iliyokwama ya viwanja vya ndege kama vya Kigoma, Shinyanga na Pemba, hali kadhalika kukarabati wa Uwanja wa Ndege Kimataifa wa Julius Nyerere Dar es Salaam (Terminal II) na mafunzo.

Pia kuna wakati kukaripotiwa kupatikana mkopo wa shilingi trilioni 1.3 uliotolewa na Shirika la Fedha Duniani (IMF) kwa ajili ya kushughulikia janga la ugonjwa Covid-19. Na unaosaidia ujenzi wa maelfu ya madarasa nchi nzima, ambayo wanafunzi wa sekondari wameripoti masomomi mwezi huu.

Inaelezwa, Rais Samia amewekeza zaidi dira ya uchumi wa nchi kupitia diplomasia ya uchumi na hata alipounda baraza la mawaziri la mwanzo, Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki likaongozwa na mkongwe wa diplomasia, mwanamama, Balozi Libarata Mulamula.

Akamwingiza kwa mara ya kwanza kwenye siasa kupitia kumteua ubunge na uwaziri, baada ya kutumikia majukumu ya kidiplomasia kwa miaka 30, ikiwamo katika majukumu ya Umoja wa Mataifa.

Hata mabadiliko aliyofanya, wizarani, jukumu la kusimamia diplomasia kimataifa ngazi ya uwaziri, leo amemkasimu mjuzi mwingine, Stergomena Tax, aliyewahi kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, pia Katibu Mtendaji wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

**AWAFUNZA MABALOZI**

Mnamo Novemba mwaka jana, Rais Samia akakutana na mabalozi wa Tanzania walioko nje ya nchi, akiwahimizia kuendana na mabadiliko ya dunia katika utekelezaji wa diplomasia ya uchumi, ili ilete tija zaidi kwa Taifa.

Ni maelekezo yake mkutanoni Zanzibar, akiwataka wahakikishe Tanzania inanufaika kiuchumi kisiasa na kijamii katika kipindi kilichopo cha mabadiliko duniani, hali inayopatikana kupitia hatua kama kubadilisha mbinu, mikakati na vipaumbele katika utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje kufikia malengo kusudiwa.

Anawakumbusha mabalozi hao kuwa, yapo masuala mapya yanayoendelea duniani, ambayo kwa kiasi kikubwa yanaiathiri Tanzania kiuchumi, hata kidiplomasia ambayo Sera ya Mambo ya Nje, inapaswa kuyazingatia, ili kwenda sambamba na mabadiliko hayo.

Pia anasema Sera ya Mambo ya Nje ya miaka 20 iliyopita inatakiwa kutathminiwa, iweze kutoa majibu katika kushughulikia changamoto hizo mpya za dunia, ikiwemo mabadiliko ya tabianchi, changamoto za afya, Mapinduzi ya Nne ya Viwanda, mabadiliko ya mwelekeo wa uchumi wa dunia, uhalifu kimataifa, kutanuka matumizi ya Kiswahili na namna ya kuwashirikisha diaspora kuchangia maendeleo nchini.

"Mabalozi naomba tuongeze uwajibikaji kwa kushirikiana na wadau wote muhimu wa serikali na sekta binafsi, ili kuhakikisha diplomasia ya Tanzania inakwenda na wakati na ufanisi," anawaelekeza Rais Samia.



# Wananchi waombwa kuiamini Mahakama

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MTENDAJI Mkuu wa Mahakama, Prof. Elisante Ole Gabriel, amewataka wananchi kuendelea kuuamini mhimili wa Mahakama kuwa unatenda haki kwa kila mtu.

Aliyasema hayo jana jijini hapo alipotembelea katika Maonyesho ya Wiki ya Sheria ambayo kitaifa yanafanyika katika viwanja vya Mwalimu Nyerere.

Akiwa katika maonyesho hayo aliwataka wananchi kuendelea kuuamini muhimili wa Mahakama kwa kuwa unatenda haki na huchukua hatua za kurekebisha pale vinapojitokeza vikwazo vya kibinadamu.

"Tuna mifumo mizuri ya kurekebishana nadhani hilo lisihamishe imani ya Watanzania kwa Mhimili wa Mahakama, ndani ya Mahakama kuna miongozo mizuri na sheria zitafuatwa, maamuzi ya kisheria hayafanyiki kiholela yanazingatia sheria, hivyo wananchi wanatakiwa kuendelea kuamini kuwa unatenda haki," alisema.

Aidha, alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutoa fedha kwa ajili ya kuboresha, kukarabati na kujenga miundombinu ya Mahakama.

Alisema kupitia mkopo wa masharti nafuu uliotolewa na Benki ya Dunia (WB) awamu ya pili serikali imeipatia Mahakama Sh.bilioni 207 kwa ajili ya kuongeza wigo wa upatikanaji haki kwa wananchi.

"Natoa shukrani za dhati kwa serikali kwa sababu inatoa fedha nyingi kwa ajili ya kuiwezesha Mahakama kuwa na miundombinu rafiki na fedha inatumika vizuri," alisema.

Alibainisha kuwa wameshajenga vituo jumuishi sita katika mikoa mitano na vingine tisa vitajengwa ifikapo mwaka 2024. "Lengo la kujenga vituo hivyo siyo kuwa na majengo bali ni kuhakikisha miundombinu ya utoaji haki inaboreshwa. Wananchi wanatakiwa kujenga utamaduni wa kufuatilia kazi zinazofanywa na Mahakama kwani serikali imebadilisha kwa kiwango kikubwa," alisema.

Naibu Katibu wa Tume ya Utumishi wa Mahakama, Enziel Mtei, alisema kwa sasa masuala yote ya utumishi kwa watumishi wa mahakama yanashughulikiwa na tume hiyo na kuna kamati za maadili ya mahakimu katika ngazi za mikoa na wilaya ambazo kazi yake ni kuchunguza malalamiko dhidi ya mahakimu.

# 'Watu 212 kila mwaka wanaugua kifafa'

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WATU 212 kila mwaka nchini hupata ugonjwa wa kifafa kunakosababishwa na kula nyama iliyoathirika na vimelea vya mnyoo tegu wa nguruwe, huku serikali ikitumia Sh. bilioni 12 kuwahudumia.

Hayo yalibainishwa juzi na Mkurugenzi wa Mtandao wa Kisayansi (CYSTINET-Afrika), Prof. Helena Ngowi, alipokuwa akiwasilisha mada kuhusu magojwa ya mnyoo tegu wa nguruwe na madhara yake kwa jamii.

Alisema utafiti huo umefanywa kwa ushirikiano na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Chuo Kikuu cha Dar es Saalam (UDSM) pamoja na Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR).

Prof. Ngowi alisema pamoja na idadi hiyo ya watu kupata ugonjwa wa kifafa, Sh. bilioni saba imekuwa ikipotea kila mwaka kutokana na nyama ya nguruwe kuteketezwa baada ya kubainika kuwa na maambukizi ya vimelea hivyo.

"Mnyoo tegu tafiti zinaonyesha kuwa amesambaa katika maeneo mengi duniani ikiwamo Amerika ya Kusini, Asia, Afrika na Tanzania ipo katika ukanda wa nchi ambazo zimeathirika sana.

"Aidha utafiti wa Shirika la Afya Duniani (WHO) na lile la Chakula (FAO) zimebainisha kuwa katika magonjwa 24 yatokanayo na chakula mnyoo tegu umekuwa namba moja kati ya magonjwa hayo," alisema Prof. Ngowi.

Alisema madhara mengine kiafya ni pamoja na kupata upofu, kupooza na kiuchumi nguvu kazi kupungua na kuteketezwa kwa nyama kutokana na maambukizi hayo. Mtafiti Mwandamizi kutoka NIMR, Kituo cha Muhimbili, Dk. Bernard Ngowi, alisema utafiti waliofanya umebaini kuwa moja ya sababu ya kuenea kwa mnyoo huo ni ufugaji holela wa nguruwe nchini.

Alisema katika maeneo mengi waliyotembelea wamebaini nguruwe wanafugwa kiholela hali ambayo inasababisha wawe katika hatari ya kupata maambukizi ya vimelea vya mnyoo tegu kutokana na kula vinyesi vya binadamu.

"Sababu nyingine ni watu kutumia vyoo kujisaidia kwenye vichaka kunachangia kwa kiasi kikubwa kusambaa kwa mnyoo tegu wa nguruwe kutokana na wanyama hawa kula vinyesi vya watu," alisema.

Alisema mapendekezo ya kisera kwa serikali ambayo wameyatoa ni pamoja na kuhakikisha kuwa watu wote wanaofuga nguruwe wanakuwa na mabanda ili kudhibiti mifugo yao na kuiondoa kwenye hatari hiyo.

Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Hezron Nonga, alisema kwa takwimu za mwaka 2022 Tanzania ina nguruwe milioni 3.4 ambao wanafugwa katika kanda mbalimbali za nchi.

Alisema kwa mwaka Tanzania imekuwa ikizalisha tani 770,000 za nyama na kati hizo tani 45,000 ni nyama ya nguruwe sawa na asilimia 5.9 ya nyama yote inayozalishwa nchini.

Alisema pamoja na uzalishaji mdogo wa nyama ya nguruwe nchini lakini bidhaa hiyo ina mahitaji makubwa sana hali inayohitaji serikali kuchukua hatua ya kudhibiti mnyoo hiyo.



Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete (kulia), akikabidhi vitendea kazi kwa mjumbe mpya wa Bodi ya Usajili Wataalamu wa Mipango Miji, Prosper Rwegerera, baada ya kuizindua jijini Dodoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kamishna DCEA ataja mbinu mbadala wanazotumia waraibu dawa kulevya

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

KAMISHNA Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti, Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), Gerald Kusaya, ametaja aina nne za dawa za binadamu ambazo zimeanza kutumiwa na waraibu wa dawa za kulevya kama mbadala wa dawa hizo. Hivyo amesema wataendelea kushirikiana na mamlaka zingine ili kudhibiti wimbi la matumizi ya dawa hizo.

Kusaya aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa alipotembelea Maonyesho ya Wiki ya Sheria yanayoendelea katika viwanja vya Mwalimu Nyerere.

Alizitaja aina hizo za dawa za binadamu ambazo zimeanza kutumiwa na waraibu wa dawa za kulevya kuwa ni Ephedrine ambayo inatumika kutibu magonjwa ya kifua, Ketamaine ya sindano na vindonge ambayo inatumika wakati wa kumfanyia mgonjwa upasuaji ili kuondoa maumivu.

Nyingine ni dawa za Tramadol ambayo inatumika kuondoa maumivu na Vallum (Diazepam) ambayo ndio inatumiwa zaidi na waraibu hao. Akizungumzia kuhusu shisha, alisema siyo sehemu ya dawa za kulevya ila kuna baadhi ya watumiaji wamekuwa wakichanganya na dawa hizo za kulevya. Aliongeza zipo taarifa kwa kuna baadhi ya vijana hao wamekuwa wakitumia pia rangi za kawaida za kupaka kwenye majengo, gundi, petroli kama mbadala wa dawa za kulevya lakini hivyo vyote havipo kwenye orodha za dawa hizo za kulevya.

Alisema mamlaka hiyo kwa kushirikiana na wadau wengine wamefanikiwa kung'amua aina mbalimbali za dawa ambazo zimekuwa zikitumiwa na waraibu hao na wanaendelea kuzidhibiti.

Aidha, alisema DCEA kwa mwaka jana wamedhibiti na kuzuia dawa hizo na wanaendelea kuhakikisha wanazizuia kwa sababu zimekuwa zikiharibu maisha ya watumiaji hao.

Alisema kuanzia Desemba 2021 hadi Desemba 2022 mamlaka hiyo kwa kushirikiana na vikosi vingine vya ulinzi na usalama walifanikiwa kukamata kilo 11,990 za dawa za kulevya hapa nchini.

Jenerali Kusaua alisema kati ya dawa hizo bangi inaongoza ikiwa ni kilo 6,900 na mirungi kilo 4,300 na kiasi kilichobaki ni aina zingine za dawa za kulevya ambazo ni heroine na cocaine.

Mkurungenzi kutoka Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, David Elias, alisema ofisi hiyo imekuwa ikizifanyia vipimo aina mbalimbali za dawa ili kubaini kama kuna aina ya dawa za kulevya.





# Kamati za h'shauri zatakiwa kusimamia vizuri rasilimali

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

KAMATI za ujenzi, uchumi na mazingira za halmashauri, zimetakiwa kusimamia vizuri rasilimali zinazopelekwa na serikali kwenye halmashauri kwa ajili ya urejeshaji wa uoto wa asili ambao umeharibika.

Kamati hizo pia zimetakiwa kutumia vizuri rasilimali hizo ili kuyarejesha mazingira katika hali yake ya awali na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ambayo yanaikabili dunia kwa sasa na kusababisha matatizo mengine ya kimazingira.

Naibu Katibu Mkuu wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Switbert Mkama, aliyasema hayo juzi kwenye kikao cha kamati hizo kutoka katika halmashauri nne za mikoa ya Mbeya na Njombe kilichofanyika jijini Mbeya.

Wajumbe hao walikuwa kutoka katika Halmashauri za Mbarali na Mbeya Vijijini kwa Mkoa wa Mbeya pamoja na Iringa na Wanging'ombe ya mkoani Njombe ambapo Naibu Katibu Mkuu huyo alisema wajumbe hao wamekuwa wazembe kwenye usimamizi wa rasilimali.

Alisema wamekuwa wakitumia vibaya rasilimali zinazopelekwa kwenye maeneo yao kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo jambo ambalo linasababisha ufanisi kwenye utekelezaji kuwa mdogo.

Alisema kamati hizo mbali na kutosimamia vizuri rasilimali hizo pia zimekuwa zikichelewa kupeleka taarifa za utekelezaji wa mradi wizarani jambo ambalo pia linakwamisha shughuli za mradi.

"Taarifa zenyewe zinakuwa dhaifu kwa maana ya kwamba haziendani na viwango ambavyo huwa tunatarajia, wengine huwa tunawapigia simu hawapatikani na wengine wanazima kwa makusudi," alisema Dk. Mkama.

Mratibu wa Urejeshaji Endelevu wa Mazingira na Uhifadhi wa Bioanuai, Dk. Damas Mapunda, alisema mradi huo unalenga kuwafundisha wananchi kufanya shughuli mbadala ambazo hazisababishi uharibifu wa mazingira.

Alisema wananchi wanafundishwa ufugaji wa nyuki, kuku na wanyama wengine ili kupunguza shughuli za uharibifu wa mazingira kwa ajili ya kujipatia kipato.

Alisema mradi huo unatekelezwa katika halmashauri saba za mikoa ya Mbeya, Iringa, Njombe, Rukwa na Katavi na kwamba wananchi wanafundishwa shughuli mbalimbali za ujasiriamali.

"Tunalenga kupunguza wananchi kujikita kwenye shughuli zinazochochea uharibifu wa mazingira, wasikate miti kwa ajili ya kuni, mkaa na shughuli zingine, wanatakiwa kujikita kwenye shughuli za ufugaji," alisema Dk. Mapunda.

Baadhi ya madiwani walioshiriki kwenye kikao hicho, walishauri serikali kuwafundisha wananchi namna bora ya kufanya shughuli za maendeleo ili waachane na uharibifu wa mazingira.

Diwani wa Kata ya Luhanga wilayani Mbarali, Baraka Leteyo, alishauri wafugaji wafundishwe mbinu mbadala ya kujenga mazizi badala ya kutumia miti ili kuokoa miti ambayo imekuwa ikikatwa kwa ajili ya ujenzi huo.

Alisema ikiwezekana wafugaji hao wafungishwe kutumia nyaya badala ya kutumia miti na kwamba hiyo itasaidia kupunguza matumizi ya miti kwenye maeneo hayo.

## Vifo vya mama na mtoto mkoani Mbeya vyapungua

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya, imesema vifo vya mama na mtoto vimepungua kutoka vifo 75 hadi 65 katika kila vizazi 1,000 kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alitaja takwimu hizo wakati wa uzinduzi wa mfumo wa dharura wa mama wajawazito na watoto wachanga ujulikanao kama M-Mama ambao unalenga kupunguza vifo vya mama na mtoto nchini.

Mfumo huo ulizinduliwa na Rais Samia Suluhu Hassan mwaka jana na kwa sasa unaendelea kuzinduliwa katika mikoa mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji.

Alisema vifo hivyo vimepungua kutokana na kuimarika kwa huduma za afya katika mkoa huo ikiwamo ujenzi wa vituo vya kutolea huduma za afya katika maeneo mbalimbali pamoja na mafunzo ya mara kwa mara kwa watumishi wa afya.

"Tunaamini kwamba mfumo huu utasaidia kupunguza zaidi vifo hivi, wataalamu wetu watapata taarifa mapema na watawahudumia kinamama na watoto wetu kwa uharaka na weledi zaidi," alisema Homera.

Homera aliagiza halmashauri zote za mkoa huo kuhakikisha zinaendeleza utoaji wa elimu kwa watumishi wengine kuhusu utekelezaji wa mfumo huo.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Rodrick Mpogolo, alisema ili mfumo huo uwe na ufanisi zaidi inatakiwa miundombinu ya usafiri iboreshwe zaidi hasa maeneo ya vijijini ili wanawake wanaobainika kuwa na matatizo wasafirishwe kirahisi.

Aliwataka Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) kuhakikisha wanaboresha miundombinu hiyo ili ipitike katika kipindi chote cha mwaka tofauti na ambavyo baadhi ya maeneo barabara huwa hazipitiki kipindi cha masika.

Mkurugenzi wa Mfumo huo wa M-Mama kutoka Wizara ya Afya, Dolorosa Duncan, alisema mfumo huo utaenea nchi nzima kwa kuuzindua katika kila mkoa.

Alisema mpaka sasa wameshauzindua katika mikoa 11 na wataendelea katika mikoa mingine nchini na kwamba mpaka kufikia Septemba watakuwa wamezindua nchi nzima na kuendelea na utekelezaji.



Wananchi wa Kijiji cha Ikombe kilichoko Kata ya Matema wilayani Kyela katika Mkoa wa Mbeya, wakifuatilia mkutano wa uzinduzi wa uwashaji wa umeme katika kijiji chao kufuatia utekelezaji wa mradi wa ujazilizi wa umeme kwenye vijiji 35 vya wilaya hiyo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Watumishi afya wakumbushwa kufanya mazoezi ya viungo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATUMISHI wa sekta ya afya mkoani Mbeya wametakiwa kufanya mazoezi ya viungo na kuepuka ulaji usiofaa ili kuepuka kupata magonjwa yasiyoambukiza ambayo yamekuwa yakiongezeka kwa kasi nchini.

Mkurugenzi wa Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya, Dk. Godlove Mbwanji alitoa ushauri huo juzi wakati wa uzinduzi wa mafunzo ya siku tisa ya huduma jumuishi mahali pa kazi.

Huduma hizo ni zile zinazozingatia faida, kanuni, sera, miongozo na mazingira wezeshi ya kugundua na kutibu magonjwa yasiyoambukiza pamoja na Virusi Vya Ukimwi (VVU) mahali pa kazi.

Alisema magonjwa yasiyokuwa ya kuambukiza yamekuwa yakiongezeka miongoni mwa watumishi wa sekta ya afya kutokana na kutozingatia kanuni za ulaji pamoja na kutoishughulisha miili yao na hivyo akawasisitiza kuzingatia vitu hivyo.

Alisema wakati mwingine watumishi hao wanashindwa kufanya mazoezi kwa sababu ya shughuli wanazofanya na hivyo akawataka kuhakikisha wanatembea zaidi kwa miguu badala ya kupanda vyombo vya usafiri. "Ukipanga ratiba ya kufanya mazoezi hutaweza kwa sababu sio utamaduni wetu sisi Waafrika, sasa mazoezi rahisi kwetu ni ya kutembea kwa miguu, unapopanda ghorofa tumia ngazi badala ya 'lift' kama hujachelewa," alisema Dk. Mbwaji. Alisema serikali kwa sasa inatumia fedha nyingi kwa ajili ya kutibu magonjwa yasiyokuwa ya kuambukiza na hivyo ili kukabiliana nayo ni kila mmoja kuzingatia mazoezi na mfumo bora wa ulaji. Alisema tatizo kubwa zaidi kwa sasa ni uzito uliopitiliza ambao ndiyo chanzo cha matatizo mengine yakiwamo magonjwa ya moyo, shinikizo la damu pamoja na presha.

Mratibu wa mafunzo hayo, Idda Siwange alisema mafunzo hayo ni sehemu ya matakwa ya Wizara ya Afya ambayo inalenga kuimarisha afya za watumishi wake kwa kuepuka magonjwa hayo yasiyokuwa ya kuambukiza pamoja na UKIMWI.

Alisema mbali na kutolewa kwa mafunzo hayo, pia watumishi hao watapata fursa ya kupima kwa hiari afya zao hasa kubaini magonjwa hayo ili washauriwe namna ya kufanya kama watabainika kuwa nayo.

Alisema wameandaa eneo maalumu ndani ya hospitali hiyo ambalo washiriki wa mafunzo hayo watakuwa wanapimwa na kutibiwa endapo watabainika kuwa wanayo.

Aliyataja baadhi ya magonjwa ambayo yanasumbua zaidi kuwa ni shinikizo la damu, magonjwa ya moyo, saratani, magonjwa ya mapafu, macho na magonjwa ya akili.



# Dk. Mwinyi akoshwa ujio wa madaktari bingwa upasuaji

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema ujio wa madaktari bingwa kutoka Marekani na Ubelgiji ni ishara njema na fursa adhimu kwa maendeleo ya sekta ya afya Zanzibar.

Aliyasema hayo jana Ikulu, Zanzibar alipozungumza na timu ya madaktari kutoka Marekani na Ubelgiji walioongozwa na Prof. Bruno Jvan Herendaw kutoka Taasisi ya Kimataifa ya ISGE.

Madaktari hao walifika Zanzibar kwa ajili ya kuisaidia sekta ya afya kuweka kitengo cha madaktari bingwa watakaofanya operesheni bila ya kumpasua mgonjwa katika Hospitali mpya ya Mkoa wa Mjini Magharibi, Lumumba.

Dk. Mwinyi alisema madaktari hao mbali ya kutoa mbinu za kibingwa pia watasaidia maeneo mbalimbali ikiwamo kutoa vifaa vya kisasa kwenye hospitali hiyo, utaalamu kwa madaktari wazawa na kuweka miundombinu sawa ya hospitali.

Aidha, DK. Mwinyi aliishukuru timu hiyo kwa kuendelea kuiunga mkono Serikali ya Zanzibar katika kuwafikishia huduma za kisasa wananchi wake.

"Dhamira ya serikali ni kuwa na hospitali kubwa ya mkoa, naanza kupata ishara ya hospitali hii itavyokuwa bora na kuleta manufaa makubwa kwa wananchi wote." Alisema Dk. Mwinyi.

Wakizungumza kwenye mkutano huo madaktari hao waliishukuru Serikali ya Zanzibar kupitia uongozi wa Wizara ya Afya ambayo walieleza kwamba walipewa ushirikiano wa kutosha tokea hatua za awali hadi kukamilika kwake.

Akizungumza katika kikao hicho, Daktari Bingwa wa Wanawake kutoka Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja, Dk. Sabra Salum Masoud, alisema walifundishwa kuhusu operesheni za matumbo kwa wanawake bila ya kuwapasua.

Alisema tangu kupata mafunzo hayo wameshughulikia kesi 17 zilizofanikiwa na kwamba kati ya kesi hizo wamepata wagonjwa watatu waliofanikiwa kupata ujauzito baada ya matatizo yao kutibiwa.

Aidha, Dk. Sabra alisema kati ya kesi 17 walizozifanyia kazi, baadhi yao ni kutoka hospitali binafsi waliofika Hospitali ya Mnazi Mmoja kusaidiwa.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akikata utepe kuashiria ufunguzi wa jengo la tatu la abiria 'Terminal 3' katika Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume Zanzibar. **PICHA: IKULU**

# SMZ yawaandalia mazingira rafiki wafanyabiashara, wajasiriamali

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema imejipanga kuweka mazingira mazuri kwa wafanyabiashara na wajasiriamali ili waweze kufanya shughuli zao katika mazingira mazuri na kujipatia kipato.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum, Masoud Ali Mohamed, wakati akifunguwa Soko la Darajani lilioko katika eneo la Mji Mkongwe wa Unguja ambalo limefanyiwa ukarabati mkubwa. Alisema katika fedha za UVIKO-19, serikali imetenga Sh. bilioni 36 kwa wajasiriamali mbalimbali kutekeleza majukumu yao ya biashara na kupata kipato kikubwa.

Alitaja juhudi zinazochukuliwa na serikali ikiwamo ujenzi wa masoko mapya katika eneo la Unguja na kuyafanyia ukarabati mengine ambayo yapo katika uchakavu.

"Tumelifanyia ukarabati mkubwa Soko la Darajani Unguja kwa ajili ya kuwawezesha wafanyabiashara wafanye shughuli zao katika mazingira mazuri na kupata kipato,"alisema.

Aidha, aliwataka wajasiriamali kuchangamkia fursa za mikopo iliyotengwa kwa ajili yao na kufanya shughuli za biashara kwa ajili ya kuwakomboa kiuchumi.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetenga fedha nyingi kwa ajili ya wajasiriamali ambapo huu ni wakati wa kuchangamkia na kuona mnazitumia kwa ajili ya shughuli za biashara," alisema.

Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Issa Mahfudhi Haji, alisema ukarabati wa soko hilo limegharimu Sh. milioni 402 hadi kukamilika kwake ambazo zimetoka serikalini.

Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Idrisa Kitwana Mustafa alisema kuwa wafanyabiashara wote waliopisha ujenzi wa soko hilo ndiyo watakaopewa nafasi ya kwanza kuendelea kufanya biashara zao sokoni hapo.

Alisema serikali ya mkoa itahakikisha kuwa wafanyabiashara hao wanafanya kazi zao kwa saa 24 ili kuendana na haiba ya Zanzibar.

# Wanahabari watakiwa kuripoti zaidi habari za wanawake

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) kimesema ili wanawake wengi wazidi kushika nafasi za uongozi, waandishi wa habari wanawajibu wa kuripoti habari zitakazowaibua kundi hilo.

Mkurugenzi wa TAMWA Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari wakati wa mafunzo maalumu ya kuwajengea uwezo wa kuripoti habari za wanawake.

Alisema kwa muda mrefu wanawake wengi wameshindwa kufikia malengo ya kushika nafasi za uongozi katika ngazi mbalimbali kutokana na dhana potofu ya kuamini wanaume pekee ndio wanapaswa kuwa viongozi.

"Nyinyi waandishi wa habari vijana mna nafasi kubwa ya kuibadili hali hii, sauti zenu ni kubwa zaidi ambazo mkizitumia vizuri tunaweza kufika tunapopataka,"alisema.

Mwanachama mwazilishi wa TAMWA Zanzibar, Fatma Aloo, alisema walianzisha chama hicho mwaka 1987 kwa kupigania haki za wanawake.

Alisema wakati wanaanzisha chama hicho walipewa majina mengi ya kuwakatisha tamaa katika harakati zao lakini hawakurudi nyuma.

Hivyo, aliwataka wanahabari hao kujiwekea malengo pamoja na kuwa watu wenye misimamo pale wanapoamua kutafuta jambo kwa maslahi ya wanawake na umma kwa ujumla.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Kupambana na Changamoto zinazowakabili Wajane Zanzibar (ZAWIO), Tabia Makame, alisema wanawake wanaotaka kuwa viongozi wanawajibu wa kujitambua na siyo kuwa warahisi kwa kila jambo.

Alisema kuna idadi kubwa ya wanawake wanaoshindwa kufikia malengo yao kwa sababu wanashindwa kujielewa na kwa hali hiyo wanajikuta wanaingia kwenye mgongano na wasiopenda kuona wanawake wakipiga hatua zaidi za kimaendeleo.

"Lazima tukubali ukweli kwamba udhalilishaji maeneo ya kazi upo lakini ni wachache wanaoweza kukubali kuacha kazi kwa kulinda heshima yao, hivyo ni lazima nyinyi vijana wadogo mjitambue," alisema.

Waandishi wa habari vijana 18 kutoka Unguja na Pemba wanaendelea kujengewa uwezo wa kuripoti habari za wanawake na uongozi kupitia mradi unaotekelezwa na TAMWA kwa kushirikiana na Shirika la NED."

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**REVERIAN .C. MODEST** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba: **S.145/92** kilichot-olewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **NYAKATO SECONDARY SCHOOL mwaka 1979 .** kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: DSM/PHQ/RB/36830/2023**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO..01.......OF 2023**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE CORNELIUS LEMA GASPER**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LATER OF ADMINISTRATIX BY UPENDO ELIAS MLAY**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 of 1963)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above-named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the **24 day of February, 2023.**

Dated at KOROGWE this 25 day of January, 2023.

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NESTORY SHIBESHI MAZINZA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TOYOTA LANDCRUISER yenye usajili namba **T 248 DEE.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**SIM/MAS/RB/35542/2023**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**CRDB BANK PUBLIC LIMITED COMPANY** anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 263 CGA - TVS KING.** Chassis namba **MD6M14PA5K4D10611.** Engine namba **AK4DK4811668.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/URA/RB/37015/2023.**

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

Ndugu **SAMSON HIDEFONCE KAJUNA** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 492 CAA.** Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **KAG/KYA/RB/252180/2021.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi au apige simu namba **0769853969.**

---

## TANGAZO LA KUPOTEA KWA PASIPOTI



**ERICK GODFREY MKINGA** Anatangaza kupotea kwa pasipoti yake yenye Namba **TAE 353328.**
Yeyote ataekaeiona atoe taarifa Kituo chochote cha polisi **TAARIFA NAMBA: IRI/IRI/RB 30960/2023.**

---

**FOMU YA HATI YA TALAKA 2**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo Wilaya KILOMBERO**
**Kituo cha KILOMBERO**
**Mkoa wa MOROGORO**
**Shauri la ndoa Na. 02/2023**
**Jina la Mdai CHRISTOPHER MARWA MWITA**
**Jina la Mdaiwa ELIZABETH CHACHA NDISI**

**KUITWA SHAURINI**
***Kanuni ya 18 ya kanuni za utaratibu wa madai katika Mahakama za Mwanzo***

Kwa **ELIZABETH CHACHA NDISI**
Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba (eleza hapa Habari za madai) anadai talaka kutokana na kutelekezwa na mdaiwa toka mwaka 2013.

Hivyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya Alhamisi Tarehe 9 mwezi 2, mwaka 2023 saa 5:00 Asubuhi na kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku y a kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi /mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** kama hutohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikathibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa amri na muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 25 mwezi 01 mwaka 2023

MAHAKAMA YA MWANZO KILOMBERO

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA YA TANZANIA.
Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Songea
Kituo cha MJINI ,Mkoa wa Ruvuma .
Shauri la Madai Na—02 /2023
Jina la Mdai VERA ALFRED MOYO
Mdaiwa MARIA RAPHAEL DUWE
KUITWA SHAURINI MDAIWA
(Kanuni ya 18 ya Kanuni za Taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)

Kwa **MARIA RAPHAEL DUWE**
Kwa kuwa Mdai /Wadai ameleta /Wameleta madai yake/yao kwamba (Eleza hapa habari za Madai
Madai ya Tsh.3,669,000=
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 30 mwezi 01 mwaka 2023 saa 2:00 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashaidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO** :Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini , Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 19 mwezi 01 mwaka 2023.

HAKIMU WA MAHAKAMA
MAHAKAMA YA MWANZO
SONGEA MJINI
SONGEA

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

LADNESS ASIFIWE MBASHA anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye usajili namba MC 203 BYD, CHASSIS NAMBA: KE7KEFPK034398 na ENGINE NAMBA: 162FMJPK034398.Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
ARU/ARU/RB/37195/2023

---

***OFISI ZA MATANGAZO***
***Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam.***
***Mobile: +255 - 745 700 710.***
***E-mail: advertise@guardian.co.tz,***
***Website: www.ippmedia.com***

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701***

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Watu 17 wajeruhiwa kwa bomu

**KINSHASA,** DRS

WAKATI watu waliojeruhiwa katika mlipuko wa bomu kwenye mji wa Kasindi wilayani Beni, wanaendelea kupata matibabu, bomu lingine limelipuka katika mji wa Beni.

Tukio hilo limetokea jana saa 12:45 katika mji wa Beni, baada ya bomu hilo lililotegwa kwenye jengo la mtambo wa kusagia unga wa mahindi pamoja na mihogo kwenye soko ya Macampagne, katika Kata ya Kalinda mjini Beni.

Walioshuhudia mkasa huo, akiwamo kijana anayefanya kazi ya kusaga unga kwenye jengo hilo, walisema kuna mwanamume mmoja aliyeweka mfuko wake wa plastiki kwenye jengo hilo na kuondoka.

Kulingana na mashuhuda ni baada ya dakika tano ndio bomu liliripuka na kuwajeruhi watu kadhaa.

Majeruhi walipokuwa wanapelekwa kwenye vituo vya afya kwa matibabu, maofisa wa Jeshi la Polisi ya Kongo pamoja na washirika wao wa polisi ya Umoja wa Mataifa, waliwasili katika eneo la tukio na kuanzisha uchunguzi, kama anavyotueleza Meleki Murara, msemaji wa polisi katika mji wa Beni.

Hata hivyo, waasi wa ADF wanashtumiwa kuhusika na mlipuko huo.

Msemaji wa jeshi la DRC, Kapteni Anthony Mualushayi, aliiambia DW, kwamba ADF wakiwa hawana uwezo wa kupambana na jeshi la Kongo, wamekuwa wakilipiza kisasi kwa kuwashambulia wananchi na kwamba, hatua madhubuti zimechukuliwa na vyombo vya dola ili kuhakikisha kwamba mashambulizi mengine hayatokei. **DW**



# Zelensky ataka vifaru vipelekwe haraka

**KYIV,** Ukraine

BAADA ya Ujerumani kukubali kupeleka vifaru aina ya Leopards 2 nchini Ukraine, kiongozi wa nchi hiyo Volodymyr Zelensky, amezitaka nchi washirika kuwasilisha vifaa hivyo haraka.

Katika hotuba yake ya jana usiku, Volodymyr Zelensky aliziomba nchi washirika kutuma makombora ya masafa marefu na ndege za kivita.

Kauli yake aliitia baada ya Marekani na Ujerumani kutangaza kutuma vifaru vya Abram na Leopard nchini mwake kwa ajili ya kusaidia vita dhidi ya Russia.

Hata hivyo, Russia imeshutumu tangazo hilo na kuita kama uchochezi wa wazi na kusema kwamba vifaru vyovyote vilivyotolewa vitaharibiwa.

Rais Zelensky alisema alimwambia Katibu Mkuu wa Nato Jens Stoltenberg kwamba lazima maendeleo yafanywe katika nyanja nyingine za ushirikiano wa ulinzi.

Alisisitiza kwamba sio kuwasilishwa kwa haraka kwa vifaru vya Magharibi, lakini pia kuwe na idadi kubwa vifaa na kikosi kitakachoweza kuzuia mashambulizi na dhuluma.

**Waziri wa Mambo ya Nje wa Russia Lavrov yuko Afrika, sio kuona emoji ya chui, lakini kudai kwa uwazi kwamba washirika wa Ukraine wanataka kuharibu kila kitu cha Russia.**

Ingawa Zelensky kwa sasa ataangazia namna ya kuhakikisha jeshi la anga la Ukraine lina ndege za kivita za kisasa.

Hata hivyo, Marekani itatuma vifaru vyenye nguvu 31 katika vita nchini Ukraine, ikiungana na Ujerumani kwa kutuma magari hayo kusaidia mapambano dhidi ya uvamizi wa Russia.

Uamuzi wa kukabidhi vifaru vya M1 Abrams ulitangazwa saa chache baada ya Ujerumani kukubali kuwa itapeleka vifaru 14 vya Leopard 2 kwenye uwanja wa vita.

Ujerumani iliidhinisha nchi nyingine za Ulaya kutuma vifaru vilivyotengenezwa nchini humo kutoka kwenye maduka au hifadhi zao.

Ukraine ilikuwa ikizishawishi nchi washirika wa Magharibi kutuma vifaa vya kijeshi kwa miezi kadhaa.

Imepongeza matangazo hayo kama hatua ya mageuzi ambayo yanaruhusu jeshi lake kupata nguvu tena na kurudisha eneo lililodhibitiwa karibu mwaka mmoja baada ya Russia kuvamia.

Pia ilisema kuwa vifaru hivyo vinaweza kusaidia kuzuia mashambulizi ya Russia katika msimu wa joto.

Katika hatua nyingine, Ofisi ya Waziri wa Mambo ya Nje ya Ujerumani, imeshutumiwa baada ya kulenga ziara ya Waziri wa Mambo ya Nje wa Russia, Sergei Lavrov, katika nchi za Afrika kama safari ya kuona chui.

Katika ujumbe wa Twitter, ofisi hiyo ilisema, "Waziri wa Mambo ya Nje wa Russia Lavrov yuko Afrika, sio kuona emoji ya chui, lakini kudai kwa uwazi kwamba washirika wa Ukraine wanataka kuharibu kila kitu cha Russia".

Wengi walikasirishwa na kauli hiyo kwamba wanyamapori wa Afrika ndio kitu pekee chenye thamani ya kumleta mjumbe wa Russia barani humo.

Ebba Kalondo, msemaji wa mwenyekiti wa Umoja wa Afrika, alishangaa na kuandika kwa kuhoji "inaonekana kama bara la Afrika, watu wake na wanyamapori ni mzaha kwako?"

Kalondo alibainisha kuwa Waziri wa Mambo ya Nje wa Ujerumani, Annalena Baerbock, alitembelea makao makuu ya Umoja wa Afrika nchini Ethiopia hivi majuzi, Je, alikwenda kuona wanyama? **BBC**



Mkazi wa Brazil, Rafael Bridi, akipita kwenye kamba yenye urefu wa mita 114 na mita 510 kutoka chini ya ardhi, akivuka mji wa Vale do Anhangabau katika jiji la Sao Paulo juzi. **PICHA: AFP**

# Waandamana kumpinga rais mpya

**LIMA,** Peru

MAELFU ya waandamanaji nchini Peru, wameingia mitaani katika mji mkuu wa Lima na kukabiliana na polisi, wakishinikiza rais mpya Dina Boluarte kuondoka madarakani.

Hata hivyo, Rais Boluarte alitoa wito wa mapatano baada ya miezi miwili ya mfululizo wa maandamano.

Maelfu ya waandamanaji waliomiminika barabarani mjini Lima, huku wakikabiliana na maofisa wa polisi kwa kurushiwa gesi ya kutoa machozi.

Maandamano ya kuipinga serikali yaliyofanyika jana nchini humo ndio yaliokuwa makubwa na yaliojaa ghasia tangu yale ya siku ya Alhamisi wiki iliyopita, wakati makundi makubwa ya watu kutoka maeneo ya Andean walipoandamana wakitaka Rais Boluarte kujiuzulu na kufanyika kwa uchaguzi wa haraka na kuvunjwa kwa bunge.

Waandamanaji wamekasirishwa na kuuawa kwa zaidi ya wenzao 40, kufuatia machafuko yaliyozuka tangu rais wa zamani Pedro Castillo, kuondolewa madarakani kwa nguvu mwezi uliopita kwa madai ya kuhusika na uasi alipojaribu kulivunja bunge. **DW**

# AZAM FC MGUU SAWA KWA DODOMA JIJI LEO

**Na Saada Akida**

HATUA ya 32 bora ya Kombe la Shirikisho la mpira wa miguu Tanzania (FA), linaanza leo kwa michezo mitano kupigwa katika viwanja tofauti, huku Azam FC wakiwa nyumbani kucheza na Dodoma Jiji na JKT Tanzania itakuwa ugenini kwenye Uwanja wa Ushirika, kumenyana na Polisi Tanzania.

Maafande wa Green Warriors watakuwa na kibarua mbele ya Mbuni FC, huku Mtibwa Sugar wakiwa Manungu Complex kumenyana na Buhaya FC.

**Mchezo wa Gwambina FC dhidi ya Pan African umefutwa baada ya timu hiyo kuondolewa kwa sababu ya sintofahamu iliyotokea kwa mmiliki wake na TFF.**


Akizungumza na gazeti hili Kocha msaidizi wa viungo wa Azam, Agrey Morris, alisema mechi hiyo itakuwa ya ushindani mkubwa kwa kuwa ni mchezo wa mtoano na wao wanahitaji kupata matokeo mazuri ili kusonga mbele baada ya kupoteza kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Maandalizi yamekamilika, tumejiandaa kuhakikisha tunafanya vizuri, tunalihitaji hili kombe ni lazima ushindi uanzie katika mchezo huo na Dodoma Jiji ni timu nzuri tumewahi kukutana nao katika ligi na mchezo unakuwa mgumu," alisema.

Aliongeza; "Tunahitaji matokeo chanya katika mchezo wetu huu kwa kuhakikisha malengo yanafikiwa na hilo wachezaji wanalifahamu, tutaingia kwa tahadhari kubwa dhidi ya wapinzani wetu."

Kwa upande wa nahodha wa Dodoma Jiji, Mbwana Khamis, alisema wamejiandaa vizuri na makocha wamekamilisha maandalizi ya mchezo huo, wapo vizuri kuhakikisha wanasonga mbele.

"Tumefuata kila kitu alichotufundisha kocha wetu, tunacho subiri muda ufike ili kila mmoja ajue anapoelekea baada ya mchezo huu," alisema Mbwana Khamis.




Mshindi wa Multibet bonus, Peter Edward Kakundi kutoka Dar es Salaam akishikilia mfano wa hundi ya Sh. 53,753,000 baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 31 kwenye mkeka wake wa multibet ya SportPesa wiki iliyopita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Rhino Rangers yaitishia nyau Yanga*

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Rhino Rangers imeipiga mkwara Yanga kuwa itakuwa na siku ngumu Jumapili kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa kwenye mechi ya 32 bora ya Kombe la FA kwa sababu imejiandaa kusonga mbele.

Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Dan Mwang'ombe, amesema kuwa Yanga kama inataka kuwafahamu wao ni nani, basi wawaulize Azam FC ambao wameshawahi kucheza nao mara kadhaa na kuwahenyesha.

"Yanga wasitudharau, sisi safari hii tumedhamiria, tumeendelea kufanya mazoezi kwa nguvu kwa ajili ya kupanda ushindi kwenye mechi hiyo ya Jumapili, hatuendi kinyonge na kwenye mechi hizi sisi tumezoea sana kuzicheza, wakawaulize Azam FC, tumeshawahi kucheza nao mara kadhaa na wamepata shida sana," alisema kocha huyo.

Aliwataja baadhi ya nyota ambao wanao kwenye kikosi kuwa ni Selemani Kibuta na Pastory Athanas ambao wamechezea klabu mbalimbali za Ligi Kuu, lakini wameshawahi kukipiga na Simba kwenye nyakati na miaka tofauti huko nyuma.

"Pamoja na kwamba tuko daraja la pili, lakini tuna wachezaji wengi wazoefu ambao wameshawahi kuzichezea klabu mbalimbali za Ligi Kuu na madaraja mengine ya chini yake," alisema kocha huyo ambaye timu yake ilicheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2013/14.

Kikosi hicho kilikuwa kikifanya mazoezi yake kwenye Uwanja wa Vita, Tabora kilitarajia kuondoka jana kwa usafiri wa barabara, kikiwa na wachezaji 22, makocha na viongozi kadhaa kwenda Dar es Salaam ambako mechi hiyo itachezwa.

Michuano hiyo inatarajia kuanza Ijumaa na baadhi ya mechi ni kati ya Azam FC dhidi ya Dodoma Jiji kwenye Uwanja wa Azam Complex, Singida Big Stars itaikaribisha Ruvu Shooting kwenye Uwanja wa Liti, Singida siku ya Jumamosi, Simba ikicheza dhidi ya Coastal Union, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, huku Jumapili Namungo ikiwa mwenyeji wa Ihefu kwenye Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa, Lindi.

## Bares amalizana na Prisons

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Timu ya Tanzania Prisons, umethibitisha kumalizana na kocha mkuu wa Mlandege FC, Mohammed Abdallah 'Bares', kukinoa kikosi cha timu hiyo akichukuwa nafasi ya Mkenya, Patrick Odhiambo aliyemaliza mkataba wake.

Bares aliyewahi kufundisha JKT Tanzania inayoshiriki Ligi ya Championships na kabla ya kurejea kwao Zanzibar kukinoa kikosi cha Mlandege ambao ni mabingwa wapya wa Kombe la Mapinduzi mwaka 2023.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa timu hiyo, Enock Manguku, alisema wamemalizana na Bares na jana alitarajiwa kuungana na jopo la makocha waliokuwapo benchi hilo la ufundi kuanza kazi rasmi ya kuinoa timu hiyo.

Alisema makubalino ya pande hizo mbili ni kuhakikisha kocha huyo anafikia kile ambacho wamekubaliana nacho cha kupambania timu hiyo inafikia malengo ya kujinusuru kushuka daraja.

"Ni kweli tulimfuata Bares amekubali na anajua kinachotakiwa kwa sasa tunashirikiana kuondoka kwenye presha kubwa ya kushuka na kutafuta matokeo katika mechi zilizoko mbele yetu," alisema Manguku.

## Chuo Mwalimu Nyerere chaibuka cha kwanza SHIMIVUTA

**Na Romana Mallya**

UONGOZI wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwl. Julius Nyerere (MNMA), umewapongeza wanamichezo wa mpira wa kikapu chuoni hapo, baada ya kuwa washindi wa kwanza katika mashindano ya Shirikisho la Michezo ya Vyuo Vya Elimu ya Juu Tanzania (SHIMIVUTA).

Naibu Mkuu wa Chuo Taaluma, Utafiti na Machapisho, Prof. Richard Kangalawe, akizungumza juzi mkoani Dar es Salaam kwa niaba ya Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Shadrack Mwakalila, aliahidi kuendelea kuwawezesha wana michezo hao.

Mashindano hayo yalifanyika jijini Mwanza na kumalizika hivi karibuni.

Alisema ushindi wa kwanza kitaifa kwenye mchezo wa kikapu ni kitu cha kujivunia na hii itaendelea kuhamasisha wachezaji kujituma zaidi katika mashindano yajayo.

"Mmejituma na kutuheshimisha kwa kurejea na kombe la ushindi wa kwanza kitaifa kwenye mchezo wa mpira wa kikapu na tunawapa motisha ili mwendelee kujituma zaidi na kukiwakilisha chuo kwenye mashindano mengine," alisema.

Pia alisema kupitia michezo mbalimbali iliyofanyika kumewezesha chuo kupata medali nane na kwamba wanajivunia ushindi wa nafasi ya 10 bora iliyopatikana kwa miaka minne mfululizo kwenye ubunifu.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### GORDON AWANIWA

CHELSEA iko tayari kuachana na nia yao ya kumnunua winga wa Everton na England chini ya umri wa miaka 21, Anthony Gordon mwenye miaka 21, huku Newcastle pia ikikataa kujiingiza katika vita vya kumnunua kinda huyo. ***(Echo)***

### ZIYECH NAYE KWENYE RADA

KLABU ya Newcastle United inamfuatilia mshambuliaji wa Chelsea, Hakim Ziyech mwenye umri wa miaka 29 kama mbadala wa Anthony Gordon kwani hawako tayari kulipa dau la pauni milioni 60 wanalotaka Everton. ***(Telegraph)***

### EVERTON INAMTAKA

KLABU ya Everton pia inavutiwa na fowadi Hakim Ziyech raia wa Morocco na wanaweza kumnasa ikiwa Anthony Gordon ataondoka. ***(Sky Sports)***

### NUNES AGOMBEWA

CHELSEA iko tayari kushindana na Liverpool katika mbio za kumsajili kiungo wa kimataifa wa Ureno na Wolves, Matheus Nunes mwenye umri wa miaka 24. ***(Telegraph)***

### EVERTON, BIELSA BASI TENA

MAZUNGUMZO ya Everton na kocha raia wa Argentina, Marcelo Bielsa kuhusu kuwa kocha wao mpya yamegonga mwamba huku kocha wa zamani wa Southampton, Ralph Hasenhuttl akiwa chaguo jingine. ***(Idependent)***

### PORRO AKARIBIA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur wanakaribia kumnunua beki wa pembeni wa Hispania, Pedro Porro mwenye umri wa miaka 23 anayechezea Sporting. ***(Guardian)***

### ARNAUTOVIC AFUATILIWA

KLABU ya Everton inamfuatilia mshambuliaji wa zamani wa Stoke City na West Ham United, Marko Arnautovic mwenye umri wa miaka 33 ambaye anachezea Bologna. ***(Telegraph)***

### CANCELO AWANIWA MILAN

AC Milan ni moja ya klabu zinazomfuatilia beki wa pembeni wa Manchester City na Ureno, Joao Cancelo mwenye umri wa miaka 28. ***(Sun)***

### GAGLIARDINI AFIKIRIWA

KLABU ya Nottingham Forest inafikiria kumnunua kiungo wa kati wa Inter Milan, Roberto Gagliardini mwenye umri wa miaka 28. ***(Calciomercato)***

### LAMPTEY KUONDOKA

MLINZI wa pembeni wa Brighton, Tariq Lamptey mwenye umri wa miaka 22, anaweza kuondoka mwezi huu na Lyon ni miongoni mwa klabu zinazovutiwa naye. ***(Fabrizio Romano)***

### TORRES KUUZWA

BARCELONA inaweza kumuuza mshambuliaji wa Hispania, Ferran Torres katika kipindi cha majira ya joto. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 alijiunga na timu hiyo akitokea Manchester City. ***(Sport)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# RASHFORD MASHINE YA KUPAMBANA – KEANE

**●●● Asifu kuimarika kwa kiwango chake, huku akiweka rekodi zaidi katika klabu...**

**LONDON,** England

MARCUS Rashford anaonekana kama "anakuwa mashine ya kupambana" kwa mujibu wa nahodha wa zamani wa Manchester United, Roy Keane.

**Mchezaji huyo wa kimataifa wa England ali dumisha kiwango chake bora kwa kuipa United uongozi katika mechi yao ya nusu fainali ya Kombe la EFL dhidi ya Nottingham Forest kwenye Uwanja wa City Ground, juzi.**

Rashford amefunga mabao 18 kwa Mashetani Wekundu msimu huu, huku Erling Haaland (31) wa Manchester City pekee akiandikisha rekodi zaidi katika klabu za Ligi Kuu England.

"Tulikuwa uwanjani wakati wachezaji walipotoka na alionekana anapambana, kila la heri kwake," alisema Keane akiambia Sky Sports.

"Anaonekana kama mashine inayojua kupambana."

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 amefanikiwa chini ya Erik ten Hag, akionesha kuimarika kwa mabao yake matano katika mechi 32 kutoka msimu uliopita.

"Wakati mwingine ni kuhusu kujiamini - ndipo anapofikia kilele sasa. Amecheza mechi nyingi kwa United na mechi kubwa kwa England katika miaka michache iliyopita," aliongeza Keane.

"Alama ya kuuliza ambayo nimekuwa nayo kwa Marcus katika miaka michache iliyopita, sasa inatoweka.

"United imekuwa na washambuliaji wazuri kwa miaka mingi na nadhani wanahitaji mtu kama huyo. Marcus lazima aseme anataka jukumu hilo kuwa mtu mkuu. Wachezaji bora hujitokeza wiki baada ya wiki. Inaonekana yuko sawa kwa sasa na anafurahia jukumu hilo, ambalo ni jambo la kufurahisha kuona."

Kwa mujibu wa Keane, Rashford amekuwa na mafanikio makubwa tangu kuondoka kwa Cristiano Ronaldo, akiwa amefunga mabao 10 katika michezo 10 kwenye michuano yote tangu kumalizika kwa Kombe la Dunia 2022, idadi kubwa zaidi ya mchezaji yeyote kwa klabu za ligi kubwa tano za Ulaya.

"Mchezaji anapoondoka kwenye klabu jukumu linakwenda kwa mchezaji mwingine," alisema Keane.

"Ana umri wa miaka 25, sio mtoto, wakati mwingine muda unapokuwa sawa unaweza kuwa tayari kwa hilo. Hapati majeraha mabaya tena kwenye paja lake. Anaonekana kuwa mahali pazuri kiakili."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,069,8

MECHI KALI
MANCHESTER CITY
VERSUS
ARSENAL
1 | 1.79
X | 3.73
2 | 3.88

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# XAVI: DEMBELE AMEONGEZA KUJIAMINI



**BARCELONA,** Hispania

XAVI alimsifu Ousmane Dembele kwa kubadili fikra zake ili kugundua kiwango ambacho ameonesha akiwa na Barcelona msimu huu.

Barca walitinga nusu fainali ya Copa del Rey kutokana na bao la kipindi cha pili kutoka kwa Dembele na kuwalaza Real Sociedad 1-0 kwenye Uwanja wa Camp Nou juzi.

Akizungumza na vyombo vya habari baada ya ushindi huo, Xavi alimsifia Dembele kwa kujiamini na ameonesha tofauti kubwa tofauti na alipoichukua klabu hiyo Novemba 2021.

"Kitu pekee ambacho tumempa Ousmane ni kujiamini. Ninamwamini sana," alisema kocha mkuu huyo wa Barca.

"Siku zote nadhani anaweza kututengenezea mambo mengi. Naona sura za mabeki wa pembeni na wanateseka. Kitu pekee ambacho kilibidi kibadilike ni maamuzi yake dakika za mwisho.

"Nina furaha sana kwake kwa sababu alipata bao la ushindi, nadhani anafurahia na ameweza kubadilisha hali yake.

"Tunajaribu kumwongoza Dembele ili afanye uamuzi bora zaidi uwanjani. Ninaona hali nzuri kwake na anaendelea kuwa mmoja wa wachezaji bora katika nafasi yake.



## Arteta hataki kushindana na Pep

**LONDON,** England

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta amesema "nisingependa" kushindana na Pep Guardiola kuwania taji la Ligi Kuu England, EPL.

Wahispania hao wawili walifanya kazi pamoja kule Manchester City, ambapo Arteta aliacha nafasi yake kama msaidizi wa Guardiola na kuwa kocha wa Arsenal mwaka 2019.

Washikabunduki hao kwa sasa wanaongoza msimamo wa Ligi Kuu kwa tofauti ya pointi tano juu ya mabingwa watetezi City wakiwa na mchezo mmoja mkononi huku wakisaka taji la kwanza tangu mwaka 2004.

"Ni hisia za kushangaza," alisema Arteta.

Kama sehemu ya makocha wa City, Arteta alishinda mataji mawili ya Ligi Kuu, Kombe la FA na mataji mawili ya EFL.

"Namtakia mema, kwa dhati na unaposhindana na mtu kama huyu, kuna kitu kinaingia kati ya hayo," aliongeza.

Licha ya kulazimika kupambana na rafiki yake, Arteta amefurahi jinsi Arsenal sasa inashindana na City kwa mataji.

"Siku zote nilitarajia kwamba itakuwa hivyo siku moja na inafanyika msimu huu," alisema kiungo huyo wa zamani wa Arsenal mwenye umri wa miaka 40.

"Hiyo haitabadilisha urafiki wowote, wakati tulionao, jinsi yeye ni muhimu katika maisha yangu, jinsi yeye ni muhimu katika taaluma yangu.

861,169/-

# MSHINDI WA BSS 2023 KUONDOKA NA MIL. 20/-

**Na Mwandishi Wetu**

FAINALI za Bongo Star Search (BSS), zinatarajia kufanyika Februari 4, mwaka huu, ukumbi wa The Super Dome Masaki jijini Dar es Salaam.

**Mshindi wa kwanza wa shindano hilo anatarajiwa kuzawadiwa Shilingi mil. 20, mshindi wa pili Shilingi mil. 3 na wa tatu shilingi milioni moja.**

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi wa Benchmark, inayoandaa shindano hilo, Rita Paulsen, amesema msimu huu umekuwa wa tofauti na misimu yote kwa kuwa wamechukuwa washiriki 10 bora wa miaka yote.

"Wamewekwa pamoja washindi waliofika 10 bora na kutengeneza mastaa wapya kwenye msimu huu wa 13, kwa malengo ya kuwapatia mashabiki wa kipindi chetu ladha mpya tofauti na vipindi vingine.

"Kuwapatia wasanii wachanga fursa ya kuonekana zaidi na jamii yetu, kuwawezesha kuwa mastaa kwa nyimbo zao wenyewe hadi sasa waliofika 8 bora wamepata nafasi ya kurekodi na kufanya video za nyimbo zao wenyewe mpya," amesema.

Aliwataja majaji walioshiriki kuchagua wasanii waliofika fainali ni Rayvany, Shilole, Fid Q, Nandy, Barnaba pamoja na Adam Mchomvu.

Kiingilio kwenye VVIP Sh. 50,000, VIP Sh. 30,000, kawaida Sh. 15,000 na kutumia app Sh. 40,000, Sh. 25,000 na Sh. 10,000.




Mkurugenzi wa Benchmark, inayoandaa shindano la BSS, Rita Paulsen (katikati), akiwa na baadhi ya majaji. **PICHA: MAKTABA**

## Nabi: Nimeanza kuupata muunganiko wa wachezaji

INATOKA UKURASA 24

"Hii mechi ni muhimu sio kwa kutafuta matokeo bali kutaka kuona wachezaji wafuate kile ninachowapa mazoezi pamoja na kuona mfumo tunaotumia na wameanza kuuelewa kwa asilimia gani," alisema.

Aliongeza, "Musonda atafanya vizuri baada ya kuzoea mazingira, naamini ni mchezaji mzuri, hata anapokuwa uwanjani namuona ana kitu kitasaidia kwenye timu katika mipango yetu," aliongeza.

Alisema pia Mamadou Doumbia anaendelea kuzoea mazingira na hivi karibuni anaamini wataingia katika mfumo na watakuwa tishio wa timu hiyo.

"Mashabiki wa Yanga wanatakiwa kupunguza presha, tumesajili wachezaji wazuri ambao watafanya vizuri na kuisaidia timu yetu katika mashindano yote, hivyo tuwe na subira," alisema Nabi.

Yanga wanajiandaa na mchezo wao wa Jumapili wa Kombe la FA dhidi ya Rhino Rangers utakaochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.




## *Kajula amrithi Barbara*



INATOKA UKURASA 24

nye Shirikisho la Soka Afrika (CAF), pamoja na kuaminika na taasisi nyingine kubwa ndani na nje ya nchi.

Barbara, yeye alichukua nafasi iliyoachwa wazi na Senzo Mbatha ambaye alitimkia Yanga.

Mtihani wa kwanza wa Kajula utakuwa kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika ambapo Simba ipo kwenye hatua ya makundi.

## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 28/01/23 | 18:00 | Hull City vs Queens Park Rangers | 2.50 | 3.30 | 2.70 |
| 02. 28/01/23 | 18:00 | Blackburn Rovers vs Birmingham City | 2.27 | 3.20 | 3.15 |
| 03. 28/01/23 | 23:00 | Getafe CF vs Real Betis Seville | 2.95 | 2.95 | 2.55 |
| 04. 29/01/23 | 14:15 | FC Twente Enschede vs Feyenoord Rotterdam | 2.75 | 3.45 | 2.40 |
| 05. 29/01/23 | 15:00 | OGC Nice vs Lille OSC | 2.95 | 3.30 | 2.35 |
| 06. 29/01/23 | 15:30 | RSC Anderlecht vs Royal Antwerp FC | 2.75 | 3.25 | 2.50 |
| 07. 29/01/23 | 16:00 | Real Valladolid vs Valencia CF | 3.10 | 3.25 | 2.28 |
| 08. 29/01/23 | 16:30 | Brighton & Hove Albion vs Liverpool FC | 2.65 | 3.50 | 2.45 |
| 09. 29/01/23 | 17:00 | AJ Auxerre vs Montpellier HSC | 2.45 | 3.30 | 2.80 |
| 10. 29/01/23 | 17:00 | Clermont Foot 63 vs FC Nantes | 2.37 | 3.30 | 2.90 |
| 11. 29/01/23 | 17:30 | Schalke 04 vs 1. FC Cologne | 2.95 | 3.40 | 2.29 |
| 12. 29/01/23 | 18:00 | Cercle Brugge vs KAA Gent | 3.05 | 3.30 | 2.29 |
| 13. 29/01/23 | 18:15 | CA Osasuna vs Atletico Madrid | 3.20 | 3.20 | 2.26 |
| 14. 29/01/23 | 18:45 | SC Cambuur vs Fortuna Sittard | 2.75 | 3.35 | 2.45 |
| 15. 29/01/23 | 19:30 | Bayer Leverkusen vs Borussia Dortmund | 2.46 | 3.50 | 2.65 |
| 16. 29/01/23 | 20:30 | RC Celta de Vigo vs Athletic Bilbao | 2.85 | 3.00 | 2.55 |
| 17. 29/01/23 | 21:00 | Boavista Porto vs Portimonense SC | 2.27 | 3.20 | 3.15 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### IJUMAA - 27/01/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 11:45 | 4554 | Newcastle Jets vs Brisbane Roar | 2.71 | 3.19 | 2.54 |
| 14:00 | 4542 | Minerva FC vs Real Kashmir | 2.03 | 3.11 | 3.48 |
| 15:45 | 2817 | Aswan vs Talaea El Gaish | 2.90 | 2.90 | 2.60 |
| 16:15 | 1464 | AL Khaleej Khor Fakkan vs Baniyas | 2.60 | 3.28 | 2.44 |
| 16:15 | 2415 | Al Ain vs Ajman Club | 1.41 | 4.46 | 6.01 |
| 16:15 | 3054 | AEK Athens B vs Kissamikos | 2.90 | 2.90 | 2.44 |
| 16:30 | 5843 | Platinum City Rovers vs Hungry Lion | 2.90 | 2.80 | 2.52 |
| 17:00 | 1345 | Jamshedpur vs Mumbai City FC | 5.19 | 4.46 | 1.46 |
| 18:00 | 3625 | Ismaily SC vs El Daklyeh | 1.96 | 3.03 | 4.27 |
| 18:00 | 5724 | AL Tai vs Al Shabab Riyadh | 4.68 | 3.62 | 1.72 |
| 19:00 | 1183 | Al Nasr Dubai vs Al Dhafra | 1.49 | 4.26 | 5.20 |
| 19:00 | 2487 | Al Sharjah SC vs Shabab AL Ahli Dubai Club | 2.12 | 3.31 | 3.06 |
| 19:00 | 3506 | Algeria vs Ivory Coast | 1.82 | 3.30 | 4.60 |
| 19:00 | 5559 | Vsnk Varazdin vs Slaven Belupo | 2.05 | 3.17 | 3.38 |
| 20:00 | 2800 | Arab Contractors vs El Ittihad Alexandria | 2.53 | 2.97 | 2.92 |
| 20:00 | 3349 | Besiktas vs Alanyaspor | 1.59 | 4.08 | 4.98 |
| 20:00 | 4455 | Akritas Chlorakas vs Karmiotissa | 2.89 | 3.31 | 2.37 |
| 20:00 | 4785 | Goeztepe vs Bandirmaspor | 2.34 | 3.32 | 2.69 |
| 20:00 | 5646 | Apollon Limassol vs Olympiakos Nicosia | 1.35 | 4.66 | 8.90 |
| 20:00 | 5876 | Miedz Legnica vs Radomiak Radom | 2.51 | 3.01 | 2.70 |
| 20:30 | 1100 | Bologna vs Spezia | 1.85 | 3.42 | 4.07 |
| 20:30 | 1201 | Karlsruher SC vs Paderborn | 2.62 | 3.61 | 2.37 |
| 20:30 | 4212 | Stellenbosch vs Cape Town City | 2.91 | 2.91 | 2.55 |
| 20:30 | 5271 | Fortuna Dusseldorf vs Magdeburg | 1.69 | 3.97 | 4.26 |
| 20:30 | 5520 | Al Wehda vs Al Fateh (KSA) | 2.72 | 3.51 | 2.40 |
| 21:00 | 2587 | Universitatea Cluj vs Rapid Bucuresti | 2.90 | 2.95 | 2.52 |
| 21:30 | 1126 | Chateauroux vs Avranches | 1.74 | 3.57 | 4.31 |
| 21:30 | 2959 | Dunkerque vs Bourg Peronnas | 2.51 | 3.20 | 2.68 |
| 21:30 | 5685 | FC Versailles 78 vs Le Puy | 1.56 | 3.62 | 5.88 |
| 21:30 | 5923 | Cholet vs FC Martigues | 2.94 | 3.20 | 2.31 |
| 22:00 | 1327 | Den Bosch vs Maastricht | 2.27 | 3.51 | 2.78 |
| 22:00 | 2429 | PEC Zwolle vs FC Oss | 1.24 | 5.67 | 9.87 |
| 22:00 | 2923 | NAC Breda vs Jong AZ Alkmaar | 2.21 | 3.36 | 2.99 |
| 22:00 | 3150 | FC Eindhoven vs Heracles Almelo | 2.89 | 3.36 | 2.27 |
| 22:00 | 3263 | Helmond Sport vs Jong Ajax | 2.47 | 3.42 | 2.58 |
| 22:00 | 3561 | Telstar vs Almere City | 2.69 | 3.27 | 2.46 |
| 22:00 | 3836 | Senegal vs Mauritania | 1.72 | 3.64 | 4.69 |
| 22:00 | 4218 | Roda Kerkrade vs Dordrecht | 1.50 | 4.21 | 5.47 |
| 22:00 | 4639 | VVV Venlo vs ADO Den Haag | 2.25 | 3.41 | 2.89 |
| 22:15 | 3732 | FC Vaduz vs FC Wil | 2.37 | 3.36 | 2.63 |
| 22:30 | 1205 | RB Leipzig vs Stuttgart | 1.43 | 4.55 | 6.13 |
| 22:30 | 2196 | Cagliari vs Spal | 1.76 | 3.49 | 4.45 |
| 22:30 | 3313 | Stal Mielec vs Lech Poznan | 3.89 | 3.47 | 1.80 |
| 22:45 | 4476 | Standard Liege vs Eupen | 1.73 | 3.67 | 4.47 |
| 22:45 | 5081 | Cove Rangers vs Ayr United | 3.05 | 3.36 | 2.18 |
| 22:45 | 5826 | Lecce vs Salernitana | 1.87 | 3.36 | 4.05 |
| 23:00 | 1264 | Almeria vs Espanyol | 2.47 | 3.19 | 2.85 |
| 23:00 | 1416 | Racing Santander vs Tenerife | 2.73 | 2.78 | 2.83 |
| 23:00 | 1638 | Lorient vs Rennes | 3.73 | 3.53 | 1.91 |
| 23:00 | 3611 | Manchester City vs Arsenal | 1.79 | 3.73 | 3.88 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Ijumaa Januari 27, 2023
Nipashe



'Rashford mashine ya kupambana' UKURASA 21



Imani Kajula (kushoto), Ofisa Mtendaji Mkuu mpya wa Klabu ya Simba. **PICHA: MAKTABA**

## Kocha Nabi: Nimeanza kuupata muunganiko wa wachezaji

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema taratibu ameanza kupata muunganiko mzuri kwa nyota wapya na walikuwapo kikosini na atakuwa na kikosi bora kitakachofanya vizuri katika michuano ya Kombe la Shirikisho Barani Afrika (CAF).

Jumatano, Yanga ilicheza mechi ya kirafiki dhidi ya Transit Camp na kuibuka na ushindi wa mabao 2-0 kwenye kambi yao ya mazoezi ya Avic Town, Kigamboni jijini Dar es Salaam, ambapo mabao yake yalifungwa na Kennedy Musonda na Stephen Aziz Ki.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi alisema anachokiangalia katika michezo hiyo ya kirafiki ni jinsi gani ya kupata muunganiko mzuri na jinsi ya wachezaji wake hasa wapya kuingia katika mfumo ambao ameanza kuutumia kuanzia raundi ya 20 ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Alisema ameridhishwa na uwezo ulionyeshwa na wachezaji wake kwa kufuata maelekezo aliyowapa mazoezini na kuendelea na mfumo mpya ambao anahitaji wachezaji wote kuwa na uwiano mzuri wa kiuchezaji.

INAENDELEA UKURASA 23

# Kajula amrithi Barbara

**Na Adam Fungamwango**

### ●●● Atangazwa kuwa Ofisa Mtendaji mpya ni mwanachama wa muda mrefu Simba ambaye...

SIMBA imemtangaza, Imani Kajula kuwa Ofisa Mtendaji Mkuu mpya wa klabu hiyo akichukua mikoba ya Barbara Gonzalez ambaye alitangaza kuachia ngazi cheo hicho mwezi mmoja uliopita.

**Taarifa iliyotolewa jana na klabu hiyo ilimesema kuwa Kajula ndiye atakayechukua jukumu hilo kwa kipindi cha miezi sita.**

Kabla ya kuwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, alikuwa meneja masoko wa Benki ya CRDB mwaka 1999 hadi 2003, baadaye kuwa Mkurugenzi wa Masoko na Biashara wa Benki ya Posta 2003 hadi 2006.

Pia alikuwa Mkuu wa Masoko na Mawasiliano wa Benki ya NMB kutoka mwaka 2006 hadi 2013.

Wasifu wake unaonesha kuwa kuanzia mwaka huo hadi anachukuliwa na Simba, ni Mkurugenzi wa Kampuni ya EAG Group.

Mbali na hilo, Kajula ni mwanachama wa muda mrefu wa klabu hiyo na amekuwa karibu na viongozi mbalimbali na waliopita na wa sasa kwenye klabu ya Simba.

Kajula atakuwa na kazi kubwa ya kuvaa viatu vya Barbara ambaye aliingia mwaka 2020 na kupatia mafanikio makubwa klabu hiyo ndani na nje ya uwanja kwa kutwaa ubingwa wa Tanzania Bara, Kombe la FA, lakini kuingia hatua ya robo fainali ya michuano ya kimataifa mara tatu, Ligi ya Mabingwa Afrika mara mbili na Kombe la Shirikisho mara moja.

Barbara pia aliiwezesha Simba kupenya na kupata marafiki kwenye klabu mbalimbali kubwa barani Afrika, huku uongozi wake pia ukiifanya kuheshimika kwe-

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >